**Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 28 Machi, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi, Assalamu Alaykum. Mhe.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hoja yangu binafsi ya kuitaka serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi (*ZAN. ID*). Naomba kuwasilisha.

**HOJA ZA KAMATI**

**Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kama tulivyoachana jana kwamba leo hoja hii tunaichangia na mchangiaji wa mwanzo ninae Profesa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, baadae Dk. Hamza Hassan Juma na baadae ajiandae Mhe. Mohammed Mbwana Hamad. Kwa hivyo, wale Wajumbe wenye nia ya kuchangia walete ili tujipange vizuri. Mhe. Makame Mshimba.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana na nimshukuru Mwenyezi Mungu kutupa uhai wa leo asubuhi kwa kuweza kuja hapa kuwaelimisha wananchi wakajua mambo yanavyoendelea ikiwa sisi ni Wawakilishi wa wananchi katika majimbo.

Mhe. Naibu Spika, ni mra nyingi sana Baraza lako hili tukufu na hasa linapotokea tatizo huwa tunaomba tuundiwe Kamati Teule na Mwenyezi Mungu anavyojua na anavyotusaidia, tunakuwa tuna wataalamu ambao wana macho ya kuona; hawana upendeleo, hawana ghamidha na mtu na tunakuwa tunashirikiana nao kwa pamoja katika kutafuta jambo lililosomwa katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, sio siri inasikitisha sana nchi za wenzetu ukienda wana *archive* nzuri zimo ndani ya *security* ambazo huwezi ukafika hata siku moja, *24 hours* unasachiwa wewe ukiingia na ukitoka, sasa hili limekosekana.

Mhe. Naibu Spika, twende sasa hivi na utandawazi bwana, tukitaka tusitake lazima tugeuke lakini tunakuwa *slow* sana. Mimi nataka niseme kitu kimoja nimnukuu katibu wangu wa Chama cha Mapnduzi Ndugu Abdulrahman Kinana, alisema kuwa tusiwe na mawaziri mizigo, narudia tena, anasema tusiwe na mawaziri mizigo. Sikusema mimi hayo amesema katibu wa Chama cha Mapinduzi ambaye mimi ndiye kiongozi wangu.

Juzi alimsema waziri wa CCM anayeshughulikia masuala ya mbuga mbuga, alisema wazi tu aliwaambia wananchi na alimsema sana hadharani na wananchi akawaambia fanyeni kazi zenu. Kwa sababu anajua kwamba chama sio mwamvuli wa maovu, chama kinafuata sera zake za utekelezaji.

Kwa hiyo, sisi Wawakilishi hapa ni mawakili wa wananchi. Katika majimbo kuna mawakili wanaotetea watu wanaonyimwa haki zao katika Mahakama hao mbali, lakini sisi ni mawakili kwa kuwatetea wananchi ndani ya Baraza lako hili tukufu. Kwa hivyo, tusihesabike kama ni wasaliti kwa sababu ni mambo ambayo yanajitokeza wazi.

Mhe. Waziri wa Fedha juzi alisema hapa tunaibiwa shilingi bilioni 16 za wavuja jasho, sikusema mimi *hansard* ipo. Waziri alisema sana hapa na akaninukuu mimi Mhe. Makame Mshimba hayupo kaondoka. Mimi nilikwenda hospitali kupeleka wagonjwa wangu, wana jimbo lazima nichelewe, kwanza nikawapeleke wananchi wangu hospitali wakatibiwe baadae waje kunipa kura mimi, hiyo ni lazima, hiyo haiepukiki. Sasa ndio mtetezi wao kwa huko sio sehemu moja tu, sehemu zote.

Mhe. Naibu Spika, lakini nataka kusema mimi nakuwa nahesabu embe ndani ya susu mna embe 50 na susu mbili mna embe 100, sihesabu baina ya chungwa na embe naomba *hansard* ikae sawa.

Mhe. Naibu Spika, kuna hizi *master, degree, PhD*, usifikirie kuna *PhD* au *master* lazima uende ukafanye *theory,* twende kwenye *practical*, *practical* ndio inayomfanya mtu aweze kuwa na utendaji mzuri na madhubuti. Sasa hizi sisi humu tukipewa tunapewa vitu vya uhakika kwa utendaji wa kazi ndio mambo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule alisema hapa hana *PhD,* hana chochote yule pale, lakini amekwenda vizuri sana watu wote wameridhika, wamepiga makofi na wamefanya *research* nzuri. Lakini leo Mheshimiwa ni aibu, tunaambiwa huyu Humud yupo ameonekana katika *area* zile za Beit-el-Ajaib ana Mzungu wake. Sasa kama yupo sheria imeshaelekeza hapa, kifungu kilichotumiwa kwao wao ni kinyume na ilivyo sasa, Mheshimiwa ume-*reference* na ndio ilivyo siku hizi sheria.

Sheria unai-*quote* katika nchi ambayo lilitokea tukio kama lile *Wallahi well and good* kamati, nakupeni *big up* kabisa. Kwa sababu mme-*reference* kesi ambazo ziko katika nchi za wenzetu nchi ambazo zinakwenda na wakati na hii ndio sheria hata Mwanasheria anajua, Mawakili wanajua, Mahakiumu wanajua, *sometime* wanahukumu kesi kwa *reference.* Sasa sisi tunangoja *reference* ya aina gani?

Mhe. Naibu Spika, historia ya Zanzibar imepotoshwa hapa imeshaharibiwa moja kwa moja huipati tena, mikataba imeelezwa humu imeibiwa, msahafu wa historia uliotoka Makunduchi nao haujulikani umepotelea wapi, bado tunafanya mchezo, *are you serious government*? Tunasema hatuko *serious* na serikali ukweli tuuseme si kitu cha mchezo. Nyaraka za serikali zipotee inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, sasa tunawaambia wananchi watizame tuna makosa kwa kuisema serikali ijirekebishe, wananchi wenyewe watachagua sasa na waangalie tangu tulipoanza Baraza hili. Wajumbe wako tumepewa majina mabaya mabaya mbali mbali, lakini Mwenyezi Mungu anabainisha siku hadi siku. Hatuna ubaya na watu sisi wakati wa chama mimi nitakwenda kukipigia debe chama wala sitoungana na Mhe. Hija Hassan, wakati mimi natengeza sera zangu aa, nitakitetea chama changu mpaka dakika ya mwisho, lakini uovu siwezi nikaufumbia macho kwa sababu ninaharibikiwa kwenye chama changu.

Leo hatuna historia Zanzibar imepotea historia tukachukue kwa Mhe. Ali Mzee Ali, haiwezekani yeye atupe historia, ni jambo ambalo litakuwa kinyume na hali halisi ana *archive* yake mwenyewe nyumbani ambayo tukisahau kitu tumfuate yeye ndio maana yake humu.

Mimi jana nimeziona nyaraka anazo; ziko hapa kaja nazo ambazo utashangaa sana, sasa hivi ndivyo inavyotakiwa leo tunashindwa. Kwa kweli nashangaa sana halafu watu wenyewe walioiba nyaraka ndio sasa vichekesho, wamenyang'anywa soksi, buti ndio zile zile *Alhamdulillah,* inasikitisha sana hawajakamatwa mpaka leo. Humoud anaranda katika nchi yetu kisiwa cha Zanzibar, jamani sisi hatuna lengo la kutaka kugombana na wenzetu, hawa ni ndugu zetu, Oman ni ndugu wa damu lakini sio mtu

atuchezee anavyotaka yeye kwa kuwa ndugu yako wewe ukae tu akuchezee? Haiwezekani akakuchezea vibaya huyo, ndio hivi sasa. Tumemuachia kaingia anavyotaka mwenyewe, kaziiba nyaraka zilizokuwa muhimu sana, kaziparaganya.

Mhe. Naibu Spika, niwasifu sana Jeshi la Polisi kwa kazi waliyoifanya na niwape hongera sana kwa hili. Kwa sababu wamefanya vitu ambavyo kwa kutaka kujiridhisha na wao katika ushahidi wao lakini *foreigner* inawaambia hapana imemzuia kwa mujibu wa sheria na ndio ilivyo. Lakini mwenyekiti wetu ametoa vitu vikali sana; ameonesha sheria ambazo walizotumia wao zimepitwa na wakati halafu leo iwe hivi hatuko *serious*. Mwanasheria siku zote huwa nasema hapa jamani wenzetu kila siku ukicha wanaangalia mifumo ya sheria, wanakuwa wanakaa wanajaribu kubadilisha.

Mhe. Naibu Spika, hii sheria ambayo wenzetu wameitumia ningeomba sana hebu tujitahidi na sisi tuiangalie tuanze kuitengeneza iwe halali katika nchi yetu, vyenginevyo vyovyote leo tumeibiwa nyaraka keshokutwa watakuja na silaha hapa. Keshokutwa watatuletea unga mwingi sana hawa, si humpekui *diplomatic* lakini Mhe. Makame Mshimba akienda nje anapekuliwa na *diplomatic* yake. Hebu tuangalieni sisi tunaogopa nini? *(Makofi)*

Mimi nina *diplomatic* nikienda kule nanyoosha mikono juu. Nimekwenda Marekani mpaka lile *screen* linakuegemea nikanyooshwa kila upande ilimradi niliegemee ati nina *diplomatic,* si sawa sawa na huyu? Ni sawa sawa na huyu Mheshimiwa ambaye sheria inamlinda. Lakini sheria haikunilinda ulaya, lakini Zanzibar sheria inamlinda. Hebu tuitizameni ndio sheria zipi, ndio maana nikasema mnanichanganya katika kichwa changu, kwani Zanzibar hasa tunatumia sheria gani, Mwanasheria hebu niambie. Zanzibar tuna-*quote* wapi sheria iwe sisi hapa tuna-*stick* sheria ah! Kwa kweli Mheshimiwa inanisikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, huku mwishoni tunaambiwa shauri, shukurani kwa Mhe. Rais ambaye kamati imepata taarifa kuwa ameahidi serikali ataichukulia hatua kuzitafuta nyaraka hizo popote zilipo. Leo tuna miaka mingapi hapa tangu tuanze kamati, tunaomba sana Mhe. Rais lakini kweli na nyinyi mmejua kama kasema kauli hiyo Mhe. Rais, au tunamtia tu humu ndani? Kama ni kweli Mhe. Rais kathibitisha tunaziomba hizo nyaraka tuzipate na kuzipata Humoud yupo, Muscat sio mbali hapo ukifumba macho tu ushafika unamkamata Humoud.

Basi namuomba sana Mhe. Rais zipatikane *alan*, haraka sana. Kwa sababu haya ndio maslahi ya vizazi vya kesho, sisi tumeshakula umri lakini watoto wetu wanataka kujua historia ya Zanzibar ilitawaliwa vipi, mashamba yalikuwa vipi, mikataba ilifanyika vipi, tutakwenda wapi; ndio maana nikasema sitaona haya kumrudia Mhe. Ali Mzee itabidi nikamtafute nikamuulize na Mhe. Ali Mzee Ali katika kamati yake teule. Nataka niwaambie ukweli nusu mme-*quote* katika ripoti ya Kamati Teule iliyopita mmepita mikondo ile ile kumbe Mhe. Ali Mzee aliyetuletea ile kamati teule ya mambo ya ardhi mimi nilishangaa. Nilifikiri katoa mwenyewe kwenye kichwa chake kumbe ame-*quote* katika historia ya Zanzibar jinsi gani ardhi ilivyokuwa, leo wenyewe mnakwenda kuchukua pesa mnakwenda kuziuza peleka kiinua miguu. *(Makofi)*

Waheshimiwa wenzangu tusifanye mchezo hili jambo ni kubwa sana, si kitu cha masihara watu wanakwenda kutuondoshea historia yetu ya Zanzibar. Halafu mimi nataka kusema kitu kimoja kama kuna nyumba ya jirani naomba sana hebu inunuliwe ile nyumba tumpe pahala pazuri yule mtu, ili pale wajinafasi kiasi ambacho ionekane *security* iko nzuri. Lakini haiwezekani nyumba kama ile au iondokane kabisa pale itafutwe sehemu nyengine yenye kuleta maana.

Vile vile nataka kuuliza swali. Je, huyu Mkurugenzi bado anaendelea au ameshastaafu? Kustaafu kwetu tuna kawaida ya kurejeshewa tena miaka miwili kama tumefanya hivyo sijui tutawaambia nini wananchi.

Jengine niseme nililoligundua humu wamesema kuchelewa kuwekwa Mkurugenzi kwa kipindi kirefu ndio inaelekeza kutokuwa na matatizo ya aina kama hii, miaka 25 mkurugenzi *open* hapana pale kwa

kweli inasikitisha. Kwa mfano, kama kule sehemu ya *press* mpaka leo hii mkurugenzi hayupo kuna *acting* tu, tunachukua muda mrefu sasa hapa watu wakorofi ndio wanapotumia nafasi, niwaombe sana mawaziri waende kwa Mhe. Rais wamwambie.

Siku moja nilisema hapa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma akanijibu akasema inakuwaje yeye mwenyewe ni vigumu, sio vigumu jamani yule binadamu ana kazi nyingi sana si mchezo kuongoza nchi hii, ana mambo mengi, ana washauri lakini sijui kama wanakwenda kumshauri.

Kwa hiyo, ninaomba sana hili suala la ku-*delay* kutokuwekwa mtu ambaye anahusika hatari yake leo nyaraka zimeweza kuibiwa katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, kamati hawajaweka sheria kali humu, sheria kali bado hawakuiweka kabisa naomba niisaidie kamati. Mimi naomba niisaidie kamati kwa kuwa hili ni kosa la jinai *evidence* yote imekamilika, angekuwepo leo Mhe. Makamu wa Pili mimi ningemwambia kwa sababu jambo kama hili inavyotakiwa awepo. Kwa sababu hapa Waheshimiwa tunataka kutoa maamuzi mazito nani atakayebeba hapa; hayupo waziri, hayupo makamu mwenyewe, sijui nani atabeba mzigo huu au Mwanasheria utabeba mzigo huu? Inaonesha hatuko *serious* hata hii kamati hatuko *serious* nayo, kwenye ripoti hii ukweli tuuseme hakuna kuficha.

Sasa unanionesha Dk. Mwinyi yeye siye asitiwe lawamani aachiwe hapo hapo, sio Makamu wa Pili. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa halafu unanioneshea kidole mimi namsema.

Mhe. Naibu Spika, hapa polisi wamekubali kama kosa lipo na wameonesha *indicators* za sehemu ambazo watu wameingia hatiani. Lakini pili kuwa mpaka leo hii wanasheria...*(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, makofi haya tunampongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kunisikia na kuja haraka sana, ili kuendeleza gurudumu hili la maendeleo. Ndio hivyo tunavyotaka viongozi wake *sharp* maana mimi jana nilitangazwa Mshimba hayuko nilitokezea mbio hapa na ndio ilivyo binadamu na maadhura yamo. Maudhura lazima tuyavumilie, sisi binaaadamu hatujakamilika siku zote tunaamka pengine vibaya, pengine tuna hili, tuna wananchi, naendelea sasa.

Mhe. Makamu wa Pili niseme tunaingia katika sheria sasa hivi ninaomba sana na wewe ndie mtendaji Mkuu; Polisi wameleza utaratibu wao wamekamilisha kamati wameeleza utaratibu wao wamekamilisha Humoud kahusika *totally* kabisa, hana kimeme Mheshimiwa. Tunaambiwa yupo tengeneza sheria akamatwe mara moja na hao wengine waliohusika waliotajwa humu tunaomba wakamatwe mara moja na kama hawajakamatwa leo hii Mheshimiwa peleka *message* kwa Polisi wakamatwe, kwa sababu ni vitu ambavyo vitakuwa kila siku tunapiga kelele. Tunaingziwa kwenye mabango sisi wengine bahati yetu ya kunguni. Lakini ndio hivyo hivyo kutokana na usemaji ukweli, hali halisi ilivyokuwa.

Kuhusu habari ya Mkurugenzi, sheria mnayo wenyewe hiyo mimi sisemi kwa sababu hili suala linaonesha, tumeelewana Mhe. Naibu Spika, hili nataka kumalizia mchango wangu, kama leo nilivyosema kuwa sitokuwa na michango mikubwa sana lakini kutokana na hali halisi ilivyo Mhe. Naibu Spika, wizara hii kwa makusudi naomba sana watafutiwe eneo ambalo litakuwa na *security* zaidi.

La kushangaza naambiwa kuwa hata dawa zile za kuzifanya zile karatasi ziwe zina uhai zimekosekanwa. Mheshimiwa wakati mwengine huwa tunapiga kelele mimi sisemi tena suala la bajeti finyu sisemi, kwa sababu si bajeti finyu. Bajeti tunakula hakuna tena bajeti finyu tunaambiwa hapa Waziri wangu wa Fedha nampenda sana, ametuhakikishia kwamba fedha Zanzibar zipo kashindwa kutwambia watu wanakula tu. Lakini sisi tumejua kama pesa zinaliwa.

Sasa leo kweli kuna vitu muhimu hivi, jengo kama lile lilikuwa halina *CCTV,* jengo kama lile linaachiwa tu huria. Mheshimiwa kwa kweli hakuna hata mlinzi zisiimbiwe nyaraka, wewe unafanya mchezo! Nasikia nyaraka moja ile *one paper* moja si chini ya dola elfu kumi, hata mimi nitaiba, asibe mtu vipi na watu wetu masikini mishahara yenyewe duni.

Lazima Mhe. Naibu Spika, kutakuwa na wizi tu hapa asikudanganye mtu. Sasa jinsi ya ku- *control* mambo haya lazima tufikie pahali tuweke mishahara ambayo inayolingana halafu mimi nataka niulize mshahara wetu ukiangalia unalingana na nchi gani, hakuna. Siku moja Mhe. Hamza Hassan Juma aliuliza swala hapa watu wengine wanamuona sijui vipi, aliuliza kweli nchi gani iliyokuwa haina kituo kikubwa cha daladala hapa kinachoishia *town*?
Mie nikajibu Zanzibar na ukiangalia kwani uongo, sasa nikiuliza mshahara wetu unalingana na nchi gani nitapata jibu gani. Huo mshahara wetu ambao hapa Zanzibar hapo *mainland* tu mshahara wa dereva ndio mashahara hapa wa waziri, hebu nambie hapo tu wala tusiende mbali. Hapa mtu ana *Diploma* na *Master* ana kila kitu anapewa mshahara sawasawa na dereva wa waziri wa *mainland* hapo.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hiyo inasikitisha sana, sasa mimi nafikiria moja katika kuzuwia wizi kuweko na mishahara mizuri.

Jengine ukiondoa adha hii tuwe na jengo ambalo litalokuwa lina *full security*. Sasa hiyo niseme kuwa ndiyo serikali ambayo sasa inajitahidi katika kuekeza. Sasa mimi nauliza wananchi namalizia malizia.

Wananchi waone sisi tunawatetea humu kwenye Baraza je, tunawatendea haki au hatuwatendei haki. Kitandawili nani anaetetea haki wananchi katika Baraza hili kati ya waziri na *backbencher,* wananchi tunaomba watupatie jibu la haraka sana. Watupatie jibu kwa sababu sisi ndiyo lengo letu hili kuiangalia serikali, kuikemea serikali iweze kujirekebisha, iweze kujirekebisha katika mambo ambayo yaliyokuwa ya hatari na namna kama hii.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na mambo mengi sana kwa kuwa leo Jumamosi nataka kumpa kijiti mwenzagu hapa Mheshimiwa, yeye sijui umpe cheo gani mie umenipa u-*professor*, mimi nakubalianja nao na u- *professor* Mhe. Naibu Spika, kwangu mimi unakubalika tena sana tu anaetaka sawa, asietaka basi. Lakini ukweli unakubalika kwa sababu jamani u- *professor* watu sijui wanatafsiri vipi. Mimi ninavyojua kuwa na uchungu wa nchi, kuwa na uchungu kwa kuwatetea wananchi haki zao ukweli haufichiki Mhe. Naibu Spika, huo ndio u- *professor.*

Sijui watu wengine wanataka uwe na *briefcase* au utembee na mavyeti ndio uonekane *professor* au uvae suti uonekane *professor,* bwana kuutetea haki kwa sheria uliyoisoma wewe.

Mimi nimesoma sheria ya uwakili ya kuwatetea wananchi kutoka jimboni ndio u- *professor* wangu niliokuwa nao mie, sina mwengine wowote siji kuzungumza maneno pumba hapa siku moja na watu wananifatilia, waniangalie natoa vitu na *evidence,* nafanya *research* kwanza *and then* nakuja huku kwa sababu humu mna sheria.

Sasa hivyo ndio lazima Mhe. Naibu Spika, mtu usisikie bwana raha mtu hujipa mwenyewe bwana. Sasa hiyo Mhe. Naibu Spika, ukweli tuuseme hivyo, mimi naomba sana niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi tuipigie debe sana hii ripoti waliohusika wakamatwe wala mimi sitaki mtu adhulumiwe, aliyetajwa humu akamatwe tu ndio aliyeiba huyo. Kwa sababu kama hajaiba hutiwi humu ndani, hata siku moja. Watu wanasema timu zimetembea sijui binani katajwa humu na mwengine katajwa humu na zote zimo kwenye *hansard,* Uingereza watu wanazisikiliza sasa hivi.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, sheria ifate mkondo wake. Kwa hayo, machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ripoti ya Kamati Teule asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Naibu Spika, nilikuwa niitikie amina.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikawa mchangiaji wa pili baada ya *professor* Mshimba kumaliza michango yake mahiri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kweli nina masikitiko makubwa sana na nina masikitiko makubwa kwa sababu kazi kubwa tunaiyoifanya, nguvu kubwa tunayoitumia, tunatumia muda wetu mwingi kufanya tafiti mbali mbali ya namna gani serikali yetu inavyoibiwa. Lakini inaonesha tafiti zile kwa kweli na bahati nzuri Baraza hili ni la wananchi kwa sababu sisi tumeletwa na wananchi wanasikia jinsi tunavyochakarika kutafuta taatifa na kuziibuwa na kuziweka hadharani.

Lakini kwa kweli hatua zinazochukuliwa na serikali kwa kweli zinakuwa zinavunja moyo sana. Leo tumekuwa tukiibiwa pesa siku zote, hatua ya mtu kumuondosha kiti hiki hapa kumuweka kiti chengine. Leo tumeibiwa nyaraka Mhe. Naibu Spika, tumeibiwa nchi.

Nyaraka ndio kielelezo cha nchi ukiwa huna nyaraka huna nchi, namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Dk. Makame Mshimba kazungumza na mimi naomba umuagize Kamishna wa Jeshi la Polisi kwanza amkamate Humoud ambaye tuna uhakika yupo Zanzibar kama jana baada ya kutajwa hajachomoka Bandarini, Viwanja vya Ndege mpaka katika yale Madiko maana yake siku hizi watu huwa wanakimbia katika yale Madiko yale ya Uvuvi; kule wanawafuata wale watu wa dago pale jamaa zangu wakojani samahani Mhe. Hamad wamvushe. Kuanzia leo pasitoke kitu. Mimi nadhani kama Humoud atatuchomoka basi kwa kweli tutakuwa hatujitendei haki.

La pili mimi nilimueelewa sana Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais alipohojiwa na kamati akasema jamani hebu twendeni taratibu ili tusiharibu mahusiano. Ni kweli kwa sababu yeye ni mratibu wa shughuli za Muungano na mambo ya mahusiano ni mambo ya Muungano.

Lakini kwa hapa Mhe. Naibu Spika, taratibu zimekiukwa huu utaratibu wa Kidiplomasia kwa sababu Diplomasia wale mabalozi na wasaidizi wao wanaokuja kuwakilisha nchi zao kwa maslahi ya nchi zao lakini wasikiuke taratibu za nchi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, tumepitisha sheria hapa kuiba nyaraka ni kosa, kuvujisha siri za serikali ni kosa, nyaraka ngapi zimeibiwa hapa hili ni kosa la jinai. Hapa hakuna mtu wa kumuachia wala wa kumuonea haya. Mimi naiomba serikali kupitia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu ndie mratibu wa shughuli za Muungano tuiombe Serikali ya Omani itoe tamko la kukanusha kuhusika na ubadhirifu huu kwa sababu huyu ni muajiriwa wa ubalozi mdogo wa Omani, Zanzibar.

Sasa kama muajiriwa, kamati imethibitisha kwa hiyo ina maana ofisi yake utajiuliza ndiyo iliyomtuma kwa sababu yule analetwa hapa na ubalozi analetwa na nchi ndiyo kazi aliyotumwa. Sasa kama ndio kazi aliyotumwa basi mimi nafikiri huo uhusiano hauna faida. Mwalimu Nyerere kuna siku alizungumzia kadhia ya ubadhifu na ufisadi, kuna kampuni moja ambayo ilitajwa sana katika sakata la *Escrow* akasema kama uwekezaji wenyewe ndio huo basi bora kurudi kwenye Ukoloni.

Kwa sababu leo haiwezekani kwamba mtu unategemea akusaidie halafu kumbe yule yule anakuja kutaka kukuangamiza. Lakini mimi ninavyoamini Serikali ya Oman, Ubalozi wa Oman hauhusiki na sakata hili. Kwa hiyo, kama hauhusiki ubalozi wa Oman na Serikali ya Oman itusaidie kumtafuta Homoud aletwe hapa ahukumuwe, apelekwe Kiinua Miguu. Yeye aliwahadaa watendaji wetu wa serikali na kuwaambia mtapata maisha mazuri. Sasa kama aliwaahidi mtapata maisha mazuri na kweli mmoja yuko Marekani Mwanaisha sijui Mwanahamisi yuko Marekani anawasiliana na wenzake kwa *WhatsApp* anawaambia nyie kaeni tu huko, na wakae kweli maana tutawapeleka Kiinua Miguu, katika hili hatuna msalie Mtume.

Hakuna Mwanahamisi, hakuna Mwatum, hakuna sijui Hamad nani, wote Kiinua Miguu, wametuibia nyaraka za siri.

Mhe. Naibu Spika, mimi bahati nzuri ni Mratibu wa Diplomasia wa Baraza la Wawakilishi na katika uratibu wangu ndio niliwapeleka Wajumbe mbali mbali, wamekwenda China kujifunza miongoni mwao ni Mhe. Ali Salum Haji, tumempeleka Mwalimu Saleh, nimempeleka Mhe. Mlinde, Mhe. Amina Idd Mabrouk wengi na tukijaaliwa tukirudi tena Barazani kuna safari nyengine za Malaysia miezi mitatu kujifunza.

Sasa ninapozungimzia ni mratibu wa mahusiano ya kimataifa ya Baraza la Wawakilishi tulipokwenda China sisi tulipata mafunzo ya mwezi mmoja; tulisoma masuala ya *Intellectual Property* tulipiga mpunga mwingi, lakini tulisoma. Moja katika mambo ambayo yanatakiwa yahifadhiwe tulisoma masuala ya *Intellectual Property,* kuna kama *Trade Market law* kuna masuala ya *Patient law* kuna *Copyright law.*

Sasa hapa kitu ambacho tulichofanyiwa sisi ni ubadhirifu katika *Copyright law,* sheria zifanye kazi na tumepitisha hivi karibuni hizi sheria. Sasa Mhe. Naibu Spika, kuibiwa nyaraka ni sawa sawa na kuibiwa cheti cha ndoa huna mke, nyaraka zimeibiwa basi lazima zitafutwe mimi nashukuru sana mapendekezo ya kamati kusema kwamba Serikali ya Zanzibar itangaze dunai nzima kumbukumbu ya nyaraka zilizoibiwa, ili kwa sababu nyaraka hizo watu watafanyia *research* watu watafanyia mambo mbali mbali, ili yoyote au chuo chochote, *professor* yeyote atakaepelekewa *research* iliyofanywa kutumia *documents* za Zanzibar; kwanza huyo mwanafunzi wake amkatalie kumpa alama mpaka amwambie nyaraka hiyo ameipata wapi, ili iweze kusaidia kupata nyaraka zetu. Sasa Mhe. Naibu Spika, hiyo ilikuwa Dijaji.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakuja sasa katika suala la kumbukumbu za nyaraka; kuna vitu sikuviona na naomba kama alivyopendekeza mwenyekiti sasa hivi iundwe kamati ya *Tripartite* Serikali, chombo cha kutunga Sheria na *Judiciary* tuendelee na hii kadhia. Hii jamani haijesha, hii hadhia kubwa. Hiki tulichokiona kidogo kuna vingi Mfalme wa Zanzibar nafikiri alikuwa na upanga upo? Kiti cha Mfalme kipo? Tusiangalie tu nyaraka, tuangalie na thamani zetu zilizoibiwa ziko duniani, watu wanatumia wanatajirika. Kwani nyie mnafikiria Humoud alivyowaambia nyie kaeni tu mtapa maisha mazuri alikuwa anasema uogo! Kwa sababu watu wanatumia dola na yule jamaa yule Fuad aliesema kaitwa pale kwenye hoteli hapo Kiembe samaki akapewa elfu ishirini atwambie elfu ishirini au Riale elfu ishirini. Maana Riale ya Oman ina thamani kuliko dola inaweza kapewa Reali elfu ishirini mwenyekiti ukasikia nimepewa elfu ishirini.

Wewe Humoud akwite akupe elfu ishirini Homoud mnamjua nyie, Homoud keshawaambia watu wataishi katika maisha bora. Tena hapa tunataka itumike ile kauli waliyopewa kamati wale waliokuwa wanalaghaiwa wamekataa, waliaombiwa hebu tutakupeni maisha mazuri kama wanavyoishi mabosi wenu. Mabosi wote wa nyaraka waangaliwe mali zao wamezipata vipi. (*Makofi*)

Mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, juzi tumepitisha sheria ya maadili, sasa unajua siku hizi kidogo nna baridi baridi huwa nachelewa kufika Barazani, sijui Mhe. Naibu Spika, kama alianza na zile sheria Mhe. Rais ambazo amezitia saini, kama bado basi tunamuomba Mhe. Rais Baraza hili kabla ya kuakhirishwa atutilie saini mswada ule tu wa maadili, watu waende mahakamani.

Chengine namuomba Mkuu wa Utumishi Zanzibar, Katibu Mkuu Kiongozi nidhamu ya watendaji wake imepunga na sisi tunasema sana na ushahidi tunatoa leo watu wale wale utasikia kaongezewa mkataba sijui kaondoshwa hapa kapelekwa hapa na kila anapopelekwa manyago. Juzi tulimsikia Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi lile jembe, maana yake akipita bwana anatuwekea sawa kila kitu anamwambia Katibu mkuu kiongozi wale wote waliotajwa katika sakata la *Escrow* watumishi wa umma wachukuliwe hatuwa. Jakaya kanyamaza kimnya anasema aaah nyie ndio mnawotunga sheria huko, watumishi Katibu Mkuu Kiongozi atajuana nao wanasiasa, kachukuwa hatua kila mmoja tumemuona.

Sisi hapa tunafumbiana macho mtoto wa mjomba, mtoto wa shangazi maana yake huyo sijui kama ukimuachisha kazi atakuwa hana jembe, kuna wakulima kule Chaani babu zangu hawajawahi kufanyakazi hata siku moja serikalini na mpaka leo wanaishi. (*Makofi*)

Leo hapa kodi za wananchi hawa tunawapa wasimamie shughuli za serikali wanatuibia. Mhe. Naibu Spika, katika hili tushaibiwa sana pesa tumestahamili lakini kwa kuibiwa nyaraka tumeibiwa utu, hatustahamili. Nataka nizungumze kitu kimoja ambacho kwa wananchi wa kawaida unajua sisi tulitawaliwa na raia kutoka Oman, mfalme wa Oman. Leo wananchi wanaposikia mfanyakazi ambaye wa ubalozi ameiba nyaraka wananchi hisia zao zitakuwa vipi huko Kwamtipura, ndio yale yale watu waliokuwa wanasema tunataka kuja kupinduliwa. Hii wataichukulia ndio maana pale nikasema Serikali ya Oman itusaidie kupitia ubalozi wake kukanusha uchafu alioufanya mtendaji wao na watusaidie vile vile kumleta, ziko sheria za kimataifa za kukamata hawa wahalifu na vitu vyengine.

Mhe. Naibu Spika, kiutaratibu wa shughuli za Serikali, mimi kidogo nilisikitika sana. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais jana ilipokuwa ripoti inasema alipohojiwa, alisema kuwa hana taarifa, mimi ninafikiri hapa lazima turekebishe utaratibu wa utendaji kazi Serikalini.

Barua inapotoka Wizara ya Mambo ya Nje, inapotoka Jeshi la Polisi kiutaratibu ipitie kwa Wizara ya Nchi ya Ofisi ya Makamu wa Pili Rais, yule ndiye mratibu wa shughuli za muungano. Haiwezekani barua inatoka kwa Kamishna wa Polisi inakwenda kwa Katibu Mkuu wa Utawala Bora, mumeona wapi? Kuna *connection* baina ya Kamishna wa Polisi na Katibu Mkuu wa Utawala Bora. Inatakiwa ipite *through* Katibu Mkuu Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu akishaipata ile inakwenda kwa Waziri, Waziri akishaipata anajua nini kilichopo, anamuarifu Makamu wa Pili wa Rais.

Leo ina maana kama Waziri wa Ofisi wa Nchi Makamu wa Pili wa Rais mpaka anahojiwa na kamati, wakati wizi huu ulianza tokea mwaka 2009 anasema hana habari. Kwa hivyo, ina maana Makamu wa Pili wa Rais ukimuuliza suala hilo na yeye atasema hana habari. Utaratibu ni lazima ufuatwe.

Naomba na mimi niliwahi kusema siku moja; jamani tufanye semina, watendaji wa Serikali wakuu, Mahakama na Baraza la Wawakilishi kuna mambo hapa yanakwenda ndivyo sivyo, matokeo yake ndiyo kama haya. Kwa hivyo naomba *correspondences* zote zinazohusu masuala ya muungano, kwa sababu hapa kiungo ni kimoja tu katika mambo ya muungano. Ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo siyo vibaya kama alikuwa hakupitishwa ofisini kwake kama Waziri hakuziona, hawezi kusema kitu ambacho hakijui.

Sasa utaratibu naomba lazima ufuatwe katika utaratibu wa Serikali. Lakini kibaya Mhe. Mwenyekiti, mwenyekiti wangu kidogo mapendekezo yote ninayaunga mkono lakini kuna moja hakulifanya; kamati hizi bwana hizi ni kamati za wananchi kuisimamia Serikali. Hapa ilikuwa itoe agizo kwa Serikali, itoe agizo maana yake kuna mapendekezo na agizo. Ofisi hii imeoza ya nyaraka. Lazima hatua zilikuwa zichukuliwe. Hapa sijaona katika mapendekezo hatua za kuchukuliwa Mkurugenzi, nani na nani. Katika kuchukuliwa hatua, ina maana hatua zikichukuliwa watahojiwa, wakihojiwa wataeleza kila kitu kilichokuwepo na kilichokuwa hakipo, lakini hata wale watumishi wa nyaraka waliofanya wizi wakahamishiwa sijui Skuli ya Kisiwandui, wale wote wachukuliwe hatua kwa sababu hiyo ni *chain* ya wizi.

Kwa hivyo naomba sana katika mapendekezo basi na hilo liwemo, wale wote waliohusika katika kadhia watendaji wa Serikali basi wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria. Unaposema kwa mujibu wa sheria, tunatumia Sheria ya Utumishi wa Umma, unapoiba nyaraka, unaposema uwongo, unafanya vitu kama hivi. Kwa hivyo hicho kitu ilikuwa kifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika udhaifu mwengine wa Serikali; leo Mkurugenzi eti baada ya nyaraka zimeshaibiwa ndiyo kauchukua ufunguo kakaa nao kwake kauficha ili nyaraka zisiibiwe, anafunga banda farasi ameshatoka. Watu wameshaiba ndiyo unachukua ufunguo. Sasa ina maana hapo ukija ukitaka sasa kuchukua hatua, ina maana kaiba yeye. Maana alipotosheka, maisha yake yameshakuwa mazuri kachukua ufunguo ili na wenzake wasipate. (*Makofi*)

Ndio, maana yake nikasema hawa waitwe wachukuliwe hatua, wahojiwe. Leo Mheshimiwa naomba tena Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais waagizwe watendaji wako wote ndani ya Serikali kuanzia sasa lazima vifanyike vikao vya *morning calls*, inaonesha Idara ya Nyaraka kulikuwa hakuna *morning calls*. Kama kungelikuwa kuna *morning calls*, ina maana vile vikao vya asubuhi kila mkuu wa idara, kila mkuu wa taasisi angekuwa anazungumza matatizo yake.

Leo matatizo yamekwenda yamekwenda kugunduliwa na kamati, sijui hakuna nini ya kuhifadhia, sijui hakuna nini, bajeti ndogo. Mambo haya yalikuwa yawe kama vikao vinafanyika. Kama hiyo Ofisi ya Nyaraka unaambiwa hicho chumba cha kuhifadhia hizo nyaraka anatakiwa awepo mtu mmoja tu. Leo ripoti inasema watu wanakwenda wanakaa, wanasukana humo humo. Eeh! jamani. Maana yake wanaiba, maana yake wanaona hakuna anayejali, wanakwenda kukaa wanasukana humo humo ndani ya chumba cha nyaraka. Mimi ninafikiri huu siyo utaratibu. Kwa hivyo *morning calls* zirudie ndani ya taasisi zetu za Serikali, ili watu waambizane kuna changamoto ziweze kutatuliwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika nyaraka ambazo sikuzisikia kuzitaja. Ninashukuru kwamba kamati imegundua kwamba ile nyaraka ya *Latham Island,* yaani Kisiwa cha Fungu Mbaraka munasema mumeikuta, *alhamdulillah*. (*Makofi*)

Mheshimiwa mgogoro uliokuwepo Tanzania na Malawi katika masuala ya raslimali. Leo wananyang'anyiana ziwa. Zamani ziwa ilikuwa aah! watu wanapita, watu wanakwenda kuvua sijui. Lakini sasa hivi inaonekana ziwa lina raslimali. Leo watu wamekwenda mpaka *UNESCO* sijui wapi Umoja wa Mataifa kwenda kutafuta. Je, hii ya wapi na hii ya wapi. (*Makofi*)

Tunashukuru alau kisiwa hiki kwa sababu kisiwa kimetiwa maneno sana na nyaraka hii ipo. Kwa hivyo sisi wala hatuna haja ya kwenda Geneva, hatuna haja ya kwenda *UNESCO* wapi, vitu vipo hivyo vilivyokuwepo viendelee kulindwa.

Kuna nyaraka Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hiki ni kitu muhimu sana. Mimi Jimbo langu ni la Kwamtipura na nilipokuwa ninasoma historia ninaambiwa kulikuwa kuna mtu akiitwa Tip Tip. Sasa Tip Tip ninaambiwa shamba lake ndiyo hilo jimbo langu.

Sasa hapa unajua kwa kuwa nyaraka zimeibiwa isipokuwa hati miliki ya jimbo anayo yeye kishapewa, eeh! bwana. Kuna nyumba karibu elfu ishirini Kwamtipura bwana. Sasa asije akaja na waraka akasema hapa itakuwa shughuli. Maana yake mimi nimechaguliwa. yeye sijui alipewa na nani.

Sasa nilikuwa ninataka nijue...kuna *document* yoyote ya tamko la Serikali kuhusu baada ya mapinduzi kutaifishwa ardhi, ipo katika *archive*? Kama haipo ya maandishi basi hata kwenye *CD* hakuna ili tuweke kumbukumbu, hiyo ndiyo hifadhi yenyewe. Lakini kuna tamko lolote la utaifishaji wa majumba. Leo alau bahati nzuri hili Baraza la Wawakilishi tumejenga jipya, lakini kama tungekuwa lile la zamani. Maana yake angekuja mtu na hati yake. Maana siku hizi watu wajanja, siku hizi wanataka kukutikisheni, mara anakuja na hati anasema Ikulu ni nyumba ya baba yake.

Sasa matamko ya utaifishaji wa ardhi, utaifishaji wa majumba, lakini vile vile na tamko la ugawaji wa eka tatu. Je, katika utafiti wenu muliofanya ipo pale *archive*, kama hakuna basi uandaliwe utaratibu ziwepo pale ili kutuhifadhia na mimi jimbo liwe salama.

Mhe. Naibu Spika, chengine kitu ambacho nilichokuwa ninataka nikiseme kwamba katika kumbukumbu hizi, kuna nyaraka muhimu sana ziliibiwa. Unajua kuna ukurasa ule wa kumi na moja kama sikosei niliona kwamba kuna nyaraka imeandikwa *Hazal. Hazal* mimi ninavyojua, unajua mimi nimezaliwa Chaani kule na akina Hamada Ali ndiyo wazee wetu wale. Nilikuwa ninasikia kwamba Hamada Ali alikuwa na *Hazal* na wapo wengine huko kama Tume kule utasikia *Hazal* wanazo. Sasa kama *Hazal* ilikuwepo wakae vimeibiwa. Leo unasikia kuna watu anakwambia ukimpa hiki kitabu cha Haza*l* anaweza akakupa mabilioni ya shilingi, maana yake *Hazal* hiyo ina shughuli kubwa. Mhe. Mohamed Aboud ananiambia anayo, basi mzee tuonane. (*Kicheko*)

Sasa Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile tuangalie haya mambo yalivyokuwa yakifanya. Hivi sasa kuna suala la tiba mbadala. Kuna waganga wa kienyeji wengi wanatoka Tanzania Bara wanakuja hapa wanatoa matangazo, wanafanya hivi na vile. Lakini kumbe pale katika *archive* tayari kuna kumbukumbu za dawa asilia.

Yaani unajua kumbe jamani pale Idara ya Nyaraka kuna hazina kubwa kweli kweli. Sasa kumbe hazina hizo zimeibiwa na inaonesha hao wengine wanaojiita ma-*professors* nani wanatibu, pengine ndiyo nyaraka zenyewe hizo hizo ambazo wanazofanyia tiba.

Kubwa zaidi, hii ripoti aliyoeleza mwenyekiti anasema kuna kumbukumbu ambayo sijui kama waliikuta au hawakuikuta, kwa sababu sikuwahi kuipitia ripoti yetu yote, inayosema kwamba kulikuwa kuna *correspondence* zinakwenda kwamba mfalme anamtuma njiwa anampa barua aipeleke kwa mfalme wa Oman. Loo! yaani unajua hawa wasanii kumbe wakiimba wanakuwa wana-*reflect* mambo mengi. Njiwa anapewa barua aipeleke kwa mfalme wa Oman.

Sasa hivi kwa wale wenzangu ambao wanatumia mitandao ya sasa hivi ya kijamii, angalia *twitter*. *Twitter* ni njiwa yule. Kumbe wale walikuwa wamemtafsiri njiwa kupitia elimu, sasa hivi wenzetu wazungu wamechukua elimu ile ile wameifanya kama *twitter*. Maana yake *twitter* sasa hivi imekuwa kama njiwa, ukimtuma hapo hapo ujumbe anaupeleka pengine.

Kwa hivyo, mimi ninadhani hizi nyaraka ambazo zimeibiwa Mhe. Naibu Spika, ni nyaraka muhimu sana ambazo kwa kweli wenzetu wamejitajirisha sana na kama wamejitajirisha, basi lazima na sisi tuhakikishe na hii itakuwa sawa sawa na *money laundering.*

Mhe. Naibu Spika, tulipitisha sisi Sheria ya *Money Laundering*. Sheria ya *Money Laundering* tuliyoipitisha, siyo suala la madawa ya kulevya, fedha yoyote unayoipata kwa njia ya ubadhirifu, ina maana baadae ukaifanyia biashara, ina maana fedha ile ume-*launder*, ina maana imekuwa safi. Kwa hivyo hawa waliohusika na kadhia hii waangaliwe sasa raslimali walizokuwa nazo kama wana *investment*.

Mhe.Naibu Spika, hapa ninaweza nikakwambia kitu kimoja. Kuna watu hapa hawalimi, hawana duka, hawafanyi biashara yoyote. Lakini wanang'ara, asubuhi mtu kamka kapiga seruni, kumbe pengine ndiyo hawa maisha bora walioambiwa na Humoud. Pengine kila mwezi anaingiziwa tu na siku hizi kuna utaratibu hapa wa fedha hizi kwenye mitandao, watu wanatiliwa pesa wee! siyo kama zile *Escrow* unatiliwa kwenye *account,* no ni kwenye simu yako umekaa nyumbani unasikia chwi! chwi! ukiangalia ni milioni tatu.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kuna watu hawa wanaotumia hizi fedha ambao fedha zile pengine wanazipata bila ya kufanya kazi, lakini kule waliibia nyaraka za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, nilichokiona kwenye ripoti hii imeelezewa hapa kuwa kuna suala zima la mawasiliano ya simu. Hapa ndiyo unapokuja ule umuhimu wa kusajili *line* zetu za simu. Bahati nzuri na ukiwa na hizi

za kisasa ukipita pahala fulani inakwambia upo katika mnara fulani, hapo upo katika mnara fulani na wale wenzetu *ZANTEL, TIGO, VODACOM* na wengine huwa wanarekodi.

Sasa hapa nimeona mawasiliano, sasa ina maana haya mawasiliano ya simu hapa unaambiwa zaidi ya mara mia moja na ishirini na saba. Kwa hivyo hapa kulikuwa kuna *connection* ya karibu, watu walikuwa wanawasiliana namna gani ya kuweza kuiba hizi nyaraka.

Sasa mimi ninadhani Mhe. Naibu Spika, kama kusema siku zote mimi ninasema, tumeshasema sana. Lakini tunasubiri, yaani tunasubiri utekelezaji wa Serikali. Mhe. Naibu Spika, na hili kama utakumbuka ilipoanza kujitokeza kadhia hii hapa Baraza la Wawakilishi, Serikali mwanzo ilikataa tusiunde Kamati Teule na Serikali ikasema aah! sisi wenyewe Serikali hili suala tunalijua tunalichunguza. Tukakataa, tukasema kama walioiba nyaraka ni watendaji wa Serikali wameshawishiwa na Humoud.

Kwa hivyo kama Serikali wao wenyewe ndiyo walioibiwa, mtu wewe bwana mwenyewe ukijiangalia hujioni, isipokuwa mpaka atokezee mwengine ndiyo akuone. Sasa leo Serikali imeunda Tume ninafikiri Tume ile ilichukua muda mrefu, sijui kama wameshatoa maamuzi.

Sasa kama Serikali baada ya sisi kuunda Kamati Teule, wakasema tunasubiri basi tunaomba katika hayo mapendekeo yao ya Serikali ambayo watampelekea Mhe. Rais kwa ajili ya maamuzi, basi na haya mapendekezo tuliyoyasema sisi, ndiyo yapewe kipa umbele.

Kwa sababu sisi ndiyo tulio-*search* tukaona kuna watendaji wamekiuka Sheria za Utumishi wa Umma, wamekiuka nidhamu ya utumishi. Hapa lazima sheria zichukuliwe. Lakini vile vile katika suala la *money laundering*, kama hawa wanamiliki biashara ambazo watashindwa kueleza wamezipata vipi, biashara hizo zifilisiwe kupitia Sheria ya *Money Laundering* ambayo tumeipitisha hapa katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, ninajua unaniangalia kwa sababu nimeshatumia muda wako mwingi, lakini kimsingi kitu ambacho ninachotaka nikiseme kwamba hapa kuna nyaraka nyingi ambazo zimetajwa ambazo ziliibiwa. Kwa kweli nyaraka hizi ndizo zinaonesha.

Mimi kwa bahati nzuri tulikuwa katika Bunge la Katiba, mimi nilitumia muda mwingi sana kusoma *documents* za Jaji Warioba. Katika *documents* za Jaji Warioba mule tuliona mpaka historia ya mfalme wa Zanzibar alivyokuwa amemiliki mpaka eneo la Moshi kule.

Mimi ninawaomba Wajumbe wenzangu ule utafiti uliofanywa na Jaji Warioba, vile vitabu tuvihifadhi, muna mambo mengi mule mazuri ambayo yatatusaidia katika utendaji wa kazi zetu. Siyo yale mapendekezo, musijemukasema Mhe. Hamza, maana yake unajua mambo yetu wakasema Mhe. Hamza bwana! ameifagilia rasimu ya Jaji Warioba, hakuna. *Documents* zilizofanywa za kitaalamu za uchunguzi ninazo, ukija nitakuonesheni lakini sikupini. Maana mtu ninaweza nikamuazima halafu akaniambia yeye haioni.

Sasa tumejaribu kuangalia kuna *documents* nyingi ambazo tokea mwaka 1859, mimi nimejaribu kuchukua sehemu ndogo tu ambayo kwa kuonesha ule umuhimu wa *documents* ambazo Serikali ya Zanzibar ilipokuwa ikifanya kazi, tokea miaka elfu moja mia nane naa. Na Jaji Warioba kule ukiangalia katika vile vitabu vyake, historia yeye aliitupa katika vile vitabu vyake kabla hiyo Tanganyika haijakuwepo, tokea ilikuwa mapande mapande ile mpaka baadae ikaja ikaunganishwa ikaitwa Tanganyika.

Kwa sasa ukiangalia vitabu kama vile inaonesha hata na wao kuna baadhi ya mambo walikwenda *archive*, ndiyo wakaweza kuyapata vile vile. Mfano kama huu ukurasa wa ishirini na tisa ambapo nitakuomba kidogo Mhe. Naibu Spika, univumilie kwa sababu ndiyo ninamalizia, hii nyaraka ambayo ya *1839*

*ARC3/12,* inasema true *copy rectification of Treaty of Ttreaty of commerce between Sayyid Said of Muscat and Queen Victoria concluded May 31, signed: by Sultan's Agents and members of East India Com and resident Resident of Persia Gulf.* Kwa hivyo, hapa inaonesha kwamba ndiyo wale waliokuwa wanasema kwamba Zanzibar utawala na ustaarabu ulianza zamani sana kwa miaka mingi sana.

Kwa sababu hata hiyo mikataba ya biashara na ndiyo maana Zanzibar sasa hivi hata ukimuona mfanyakazi wa Serikali, basi mfanyakazi yule wa Serikali aidha atakuwa na kiduka au anauza japo kuni. Kwa sababu sisi tuna historia. Angalia ukurasa wa 29, yaani ukurasa 29 yenyewe ya hiui kitabu ule ulioandikwa kwa penseli ile chini huku, mutaweza kupata idadi ya nyaraka ya 23, ni kiambatanisho, samahani siyo ukurasa ni kiambatanisho 29.

Vile vile kuna *1840 ARC3/13,* inasema *true copy rectification of Treaty of Commerce between Sayyid Said of Muscat and Queen Victoria* concluded *by May 31, signed by British Witness*. Yaani imesainiwa *document* hiyo chini ya ushahidi wa British. Kwa hivyo ina maana hii inaonesha kwamba utawala Zanzibar ulianza siku nyingi sana na hizo zote ninazozisoma siyo kama wamezikuta, hizo ngoma hawakuzikuta, wamekuta kumbukumbu tu.

Sasa vitu kama hivi ndivyo vinatakiwa viwepo. Lakini vile vile kuna *1859 ARC3/14* ambayo pia vile vile haipo, inasema *treaty of Amity, Commerce and Nevigation, between senates of the Hanseatic Republics and Majidbin Said, Zanziba, and June 1859.* Kwa hivyo ina maana hizi ni kumbukumbu muhimu.

Mhe. Naibu Spika, leo kuna watu wanafanya *research*, wanafanya *PhD*, lakini ninamshukuru sana miongoni mwa viongozi waliokuwa wamefanya *research* hizo ni viongozi wetu wa Zanzibar, akiwemo Rais Mstaafu Dk. Salmin Amour.

Kwa hivyo, ina maana vitu kama hivi, kama katika *research* yake ameshapewa *assignment* na *professor* wake, anakwenda anajua nitavikuta kwenye *archive* ya Zanzibar hakuvikuta, ina maana huyu mtu sasa unampa tabu, unamchukulia apate muda zaidi wa kuhangaika kupata *document* hizo ambazo sio rahisi kuwe kuzipata sehemu nyengine yoyote.

Vile vile kuna *1887 ARC3/15* inasema *treat of commence between empire of Australia Hungry and Baraghash bin Said Zanzibar August 11, 1887*.

Kwa hivyo, ina maana kuna mikataba mingi ambayo ni ya kibiashara, kwa hivyo ina maana Zanzibar na ndio maana tukaambiwa kwamba baada ya Mapinduzi Serikali ya Zanzibar ilikuwa ina fedha nyingi za kutosha, kwa sababu kumbe kulikuwa kuna mikataba mingi ya kibiashara, ambapo katika mikataba hiyo *of course* Zanzibar ilikuwa ina fedha zake pengine sehemu mbali mbali duniani.

Kubwa zaidi Mhe. Spika, ambalo hili ni historia nzuri ya nchi yetu. Mhe. Makame Mshimba alizungumza vizuri, *professor* Mshimba. Alizungumza kwamba sasa hivi historia ya Zanzibar inapotoshwa. Leo kuna ma-*tour guides* kule, sitaki kutaja makabila, maana nikitaja makabila ungesema aah! Basi hata na Mmasai na yeye anajua historia ya Zanzibar, lakini ndio ma-*tour guides* wetu. Unamkuta kapiga rubega lake kachukuwa watalii anakwenda nao anawaelezea historia ya Zanzibar, hili ni tatizo Mhe. Spika.

Kwa hivyo, hapa

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, malizia umeshachukua nusu saa.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Haya, namalizia mheshimiwa unajua nilikuwa nataja hizi muhimu.

Mhe. Naibu Spika, hii ya *1897 ARC3/31 slave leaflate published by British and Foreign Anti- Slavery Society. Act.1897*. Kwa hivyo, ina maana hapa inaonesha tokea mwaka 1897, tayari kuna Jumuiya zilikuwa zikipambana na biashara ya utumwa, kwa hivyo na utumwa ulianza zamani sana. Ndio maana sisi wengine leo ukitafuta *origin* yetu huikuti, kwa sababu kumbe tokea mwaka 1897 tayari wazee wetu walikuwa ni watumwa wanachukuliwa. Kwa hivyo, ina maana kuna Jumuiya ambazo zilikuwa zikipambana na ile biashara ya utumwa.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa, kama nilivyosema mwanzo, namuomba sana Kiongozi wetu wa Shughuli za Serikali, nasikitika sana kadhia hii ilipokuwa ikishughulikiwa alikuwa hapewi taarifa. Lakini kwa kuwa sisi wasemaji wa wananchi, wawakilishi wa wananchi ndio tunampa hizi taarifa kabili, ambazo zilifanywa kwa utafiti wa kina. Tunataka Humoud atafutwe, akamatwe na aulizwe ni nani aliyemtuma aje aibe nyaraka za serikali. Kwa sababu kama yeye aliwaahidi watu watapata maisha mazuri. Sisi bwana maisha mazuri tuliambiwa na Jakaya Mrisho Kikwete, tena alitangaza kwenye ilani zake wakati wa kampeni za uchaguzi, akasema maisha bora kwa kila Mtanzania.

Ni kweli vikundi vyetu mbali mbali vimepata mikopo ya AK na JK, vikundi vyetu mbali mbali vimepata misaada mbali mbali, kina mama wameanzishiwa benki yao ya wanawake. Kwa hivyo, maisha bora kwa kila Mtanzania, sisi tulitangaziwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Lakini leo Humoud anawatangazia wafanyakazi wa serikali wa Idara ya Nyaraka, kwamba atawapa maisha bora, sasa hayo maisha bora Humoud ana pesa kiasi gani, kazipata wapi na kapewa na nani, na hizi nyaraka ambazo kaziiba katumwa na nani, hili ni lazima katika hiyo hukumu. Tena naomba siku hiyo atakayokamatwa redio itangaze, halafu siku ya kesi yake tutangaziwe. Kwanza tukamuone huyo Humoud sura yake, maana wengine wala hamumjui, halafu aseme hadharani katumwa na nani, aje kuiba nyaraka za serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini naiomba tena serikali katika hili tukilifumbia macho, kama nilivyosema nyaraka ndio uhai wa nchi, ndio *existence* ya nchi, ndio uwepo wa nchi. Unapokosa vitu hivi ina maana tayari wakati wowote unaweza ukanyang'anywa hiyo nchi. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kutoa hayo maoni. Naunga mkono hoja, pamoja na yale mapendekezo niliyoyaongeza katika Kamati.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwenyekiti atakapokuja kufanya majumuisho, aseme kwamba naomba kutoa hoja kwamba hotuba hii au ripoti hii ipokelewe pamoja na mapendekezo yalioongezwa na wajumbe. Kama lipo alilolikataa aseme, kwa sababu tukijakupitisha hii ina maana tumeshaipa serikali kwenda kuyafanyia kazi. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia asubuhi hii kuwepo hapa, kwa madhumuni yale yale ya kuwatetea wananchi kuitetea nchi, pamoja na kuielekeza serikali katika yale mambo yanayofaa ndani ya nchi yetu na yale yasiyofaa na yanayofurahisha katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kukupongeza wewe kwa kunipa fursa ya angalau na mimi kusema machache katika kadhia hii ilioko mbele yetu, jambo ambalo kwa kweli linasikitisha sana. Lakini nisiwe mchache wa fadhila hata kidogo. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka, kwa umahiri wake wa kusoma ripoti hii kubwa, kwa ufasaha na kwa umahiri wa hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya mukalima huo nianze mchango wangu kwa tamko la msiba, *Innalillah Wainnaillah Rajiun.* Nasema haya kwa sababu Mhe. Naibu Spika, neno lolote la msiba au la huzuni, lazima tujipeleke kwa Mwenyezi Mungu na hili ni neno la huzuni.

Mhe. Naibu Spika, neno nyaraka watu wengi wanaweza kukosa ufahamu au kujua umuhimu hasa wa nyaraka ni nini. Hata baadhi ya wajumbe wako wanaulizana kwamba aah! hizi zimeibiwa vipi, kwani nyaraka gani. Hapa ni kuonesha kwamba kuna watu wengi wanashindwa kujua umuhimu wa nyaraka. Nahisi kwamba hata wasikilizaji wetu huko nje, miongoni mwao wanaweza kujiuliza, hivi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi leo wanazungumzia kuhusu habari ya nyaraka, badala ya kuzungumzia masuala ya maendeleo na mambo mengine. Lakini wako wanaojua umuhimu wa nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, nyaraka za serikali ndio serikali, kwa sababu bila ya nyaraka na kumbukumbu muhimu za serikali basi itakuwa tuko hewani. Mhe. Naibu Spika, kitendo cha wizi wa nyaraka, tunapaswa Wazanzibari tukilani kwa nguvu zetu zote, hili halikuwa jambo zuri na ni jambo ambalo limetunyima raha na limetunyima starehe mbali mbali za kinafsi, kutokana na kuibiwa kwa nyaraka za nchi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba waliotuhumiwa na wizi wa nyaraka, niungane na wasemaji wa mwanzo, kwamba hawa watafutwe wakamatwe na wawekwe kizuizini mara moja, mpaka tujuwe kwamba nyaraka hizi wamezipeleka wapi, ziko wapi na kwa madhumuni gani ya kuzichukua nyaraka hizi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nasikitishwa sana na watumishi au wafanyakazi wanaofanyakazi katika Idara ya Nyaraka, na nisikitike sana na hawa wanawake wawili ambao kwa kiasi kikubwa sana, ni miongoni mwa chanzo cha kuibiwa nyaraka hizi. Takriban wanawake ni waaminifu na wanawake wengi tunawaamini wanapopewa dhamana kwamba wanaweza wakazitunza dhamana zao vizuri, lakini kwa masikitiko makubwa. Sijui na wanawake waliomo ndani ya Baraza la Wawakilishi, watawachukulia vipi wanawake hawa ambao kwa kiasi kikubwa wamepitisha nyaraka hizi kwa mkono wa nyuma.

Kwa kweli hawa wanawake Mwanahawa Abdalla Ali na Mwanakombo Ali Haji, wanawake hawa niseme kwamba wamewapa picha mbaya sana wanawake wenzao wa Kizanzibari.

Mhe. Naibu Spika, wanawake wa Zanzibar ni waaminifu kiasi ambacho, tunawaamini kuwapa nyadhifa tofauti tena kubwa kubwa. Hawa wanawake wawili wanapewa dhamana ya kutunza nyaraka, halafu wanazitoa kwa mkono wa nyuma. Kwa kweli wanawake mnahitaji sana kuwapa maelekezo na maelezo wanawake wenzenu hawa, ili wakutoweni katika aibu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba tatizo ambalo limetokea Zanzibar, labda ni kutokana na kuwavumilia waovu, tunapowavumilia waovu basi yanaweza yakatokea maovu makubwa zaidi. Siku zote Mhe. Naibu Spika, Baraza lako la Wawakilishi wajumbe wengi wanapiga kelele juu ya upoteaji wa fedha, juu ya matumizi mabaya ya fedha na juu ya matumizi mabaya ya rasilimali za nchi, lakini tumenyamaza kimya. Leo inachukuliwa nchi ndani ya mkoba inapitishwa nyuma inapelekwa kwa Humoud. Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo, "usipoziba ufa utajenga ukuta".

Mhe. Naibu Spika, tunaibiwa pesa kila mwezi, leo tumeibiwa nyaraka na kesho tutaibiwa siye, hilo si tatizo jamani, tutaibiwa na kwa nini tutaibiwa, kwa sababu hakuna hukumu yoyote inayochukuliwa kwa mwizi wa mali ya umma Zanzibar. Leo nyaraka zimechukuliwa, nyaraka ambazo ndio rasilimali kubwa ya nchi. Nataka nitowe historia moja fupi.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni nchi yenye historia kubwa, inasemekana katika vitabu vya historia, inawezekana miongoni mwao ndivyo vilivyoibiwa, kwamba hata Uislamu Zanzibar umeingia kwanza

kuliko Madina. Angalia nchi ya Makka na Madina ilivyo karibu, Makka na Madina ziko karibu zaidi, kuliko Makka na hapa Zanzibar. Lakini baada ya Uislamu kufika Makka basi ulifika Zanzibar, inawezekana kwamba hata vitabu vinavyoelezea historia ya namna hiyo, Mwanahawa na Mwanakombo wamempa Humoud.

Mhe. Naibu Spika, tunahitajika viongozi wa Zanzibar kuwa makini na wala Zanzibar tusiifanye kama dutu. Dutu ni ngoma ndogo ambayo inapigwa ile dutu kwa kigongo. Kila mwenye gongo lake apige Zanzibar, jamani Zanzibar tusiifanye dutu, Zanzibar ni nchi ambayo inaheshima kubwa, sasa tusimuachie kila mwenye gongo akaipiga Zanzibar. Aliyepewa dhamana ya pesa tia pua hii na hii haipati, aliyepewa dhamana ya nyaraka pitisha mlango huu, huu haupiti.

Mhe. Naibu Spika, tunahitajika sana kujifunza na tujifunze kutokana na makosa. Unapodokolewa vitu vyako vidogo vidogo na watoto wako nyumbani na ukanyamaza kimya, basi kesho watadokoa kikubwa nyumbani, keshokutwa watadokoa kwa jirani na keshokutwa watadokoa kwa mwengine. Hawa wadokozi wadogo wadogo hawa Mhe. Naibu Spika, umefika wakati tuwazuwie udokozi na kuzuwia udokozi ni kuwadhibiti katika sheria zetu za Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha sana na niseme kwamba katika ripoti ambayo ameisoma Mhe. Mwenyekiti, wa kamati mimi nataka nizungumzie kidogo; kwanza nisome kiambatisho namba 2 katika ukurasa wa 4 wa viambatisho. Hii ni barua iliyotoka kwa Kamishna wa Polisi. Mhe. Naibu Spika, nitakachokisoma hapa ni mambo machache kiasi, uchache wake ni wa maneno lakini mantiki yake ni kubwa. Matokeo ya ukaguzi, sitaki niisome barua yote. Ukaguzi uligundua mambo yafuatayo.

Kwanza *AB record series Arabic correspondence* makasha matatu, nyaraka zote zimeibiwa, hatujui kwamba makasha haya yalikuwa na nyaraka ngapi ngapi, makasha matatu nyaraka zote zimeibiwa.

Namba *2 ZA Records Series Arabic Manuscript* zilikaguliwa na kubainika kwamba ZA 2 vitabu 9 vimeibiwa na ZA 3 vitabu 3 vimeibiwa. Mhe. Naibu Spika, tukienda katika nambari *3 AA consular records series AA4* makasha mawili yameibiwa, makasha haya yalikuwa na vitabu vingapi.

Mhe. Naibu Spika, huu mtiririko natoa kwa ufupi tu lakini ni mrefu, niseme kwamba vitabu au nyaraka zilizoibiwa ni nyingi, wala hatuwezi kuzijua kwa haraka idadi yake. Niseme kwamba kamati pale mwanzo ilipewa siku saba tu kufanyakazi, lakini baadaye walikwenda katika kazi kwa wiki sita, pamoja na wiki sita ambazo wamefanyakazi inaelekea kwamba walichokiripoti ni nusu tu ya uhalisia ambao labda ungetokea kama wangepewa muda mkubwa zaidi.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tuseme kwamba nyaraka zilizoibiwa ni nyingi na nyaraka muhimu katika nchi. Kwa hivyo, ipo haja Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilielekeze suala hili ilikamate kwa magego, vyenginevyo tujiandae na sisi kuibiwa na Humoud au mwenziwe Humoud.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba moja katika jambo la kulizingatia kabisa mtu ni kudhibiti rasilimali yake, na miongoni mwa rasilimali ya nchi ni nyaraka. Mhe. Naibu Spika, angalia nyaraka zako binafsi, cheti chako cha kuzaliwa ni waraka wako, kitambulisho cha Uzanzibari ni waraka wako, kitambulisho cha kupigia kura ni waraka wako, nyaraka za kununua viwanja nyumba na mambo mengine ni mali yako.

Angalia basi nenda nyumbani ukute kimepotea kimoja au viwili au vyote utajisikiaje. Kwa hivyo, tunapaswa Wazanzibari tuwe makini, tuangalie kipi tufanye katika kudhibiti rasilimali yetu ya nyaraka. Tujiangalie Mhe. Naibu Spika, tumejikwaa wapi. Jamani kujikwaa sio kuanguka ni kwenda mbele. Kama tumejikaa tuangalie tumejikwaa vipi ili tuweze kudhibiti mambo yetu, tuweze kudhibiti kila kilicho chetu, tutafute vizuri vije hapa, vizuri vya hapa tusivitowe kwenda nchi nyengine au kwenda pahali pengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli niseme kwamba miongoni mwa yanayo tuharibia, ni kuondoa utamaduni wetu ni kuudharau utamaduni wetu, utamaduni wetu tunapoudharau basi kila kitu kinajidharau.

Mhe. Naibu Spika, nataka nitowe mfano, mwaka juzi nilipata safari ya kwenda Zimbabwe na wenzangu, kina Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Omar Ali Shehe na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Watu wanavyoulinda utamaduni wao, tumekwenda hoteli moja pale. Wewe kama ni Rais, waziri, katibu, moja katika utamaduni wa hoteli ile ni kuvaa rubega ya kitenge, sote tumevalishwa rubega ya kitenge, watu wanatunza utamaduni wao. Lakini tumetoka Zimbabwe tunakwenda Botswana mpakani baina ya Botswana na Zimbabwe pale kama Rais, kuwa nani unashuka gari kuna sehemu lazima upite kwa miguu, kuna maji fulani ukanyage, unajua ni utamaduni wao. Sisi tumekosa kuutunza utamaduni wetu, tutaibiwa kila kitu kwa sababu tumekosa kutunza utamaduni wetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mwisho niseme kwamba kuurejesha utamaduni wa Zanzibar katika uhalisia wa Uzanzibari ni kitu muhimu, tutakapobeza utamaduni wetu basi kila baya linaweza likatushambulia hapa, Mwenyezi Mungu atukinge na kila baya.

Mhe. Naibu Spika, ahsante ninakushukuru. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Mohamed Mbwana Hamad:** Mhe. Naibu Spika, nauunga mkono ripoti ya Kamati Teule ya Uchunguzi wa Upotevu wa Nyaraka kwa asilimia mia moja kamili.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:**Tunakushukuru kwa kukumbukia. Sasa nafasi tunampa Mhe. Hija Hassan Hija, baadae Mhe. Wanu Hafidh Ameir na ajiandae Mhe. Mohamed Haji Khalid.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii ili niweze kutoa mchango uliokuwepo kwenye Kamati Teule iliyoongozwa na kaka yangu Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mwakilishi makini wa Jimbo la Kikwajuni ambaye ndiye aliyekuwa mwenyekiti wa Kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze kwa jinsi ilivyofanya kazi kwa muda mfupi na wakatoa taarifa ambayo ina mapungufu kwa sababu ya muda, lakini kwa kweli inaonesha picha halisi ya jambo hilo lilivyotokezea hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niwapongeze Wajumbe wa Kamati hii na niwapongeze Makatibu waliosaidia kwa utaalamu kwenye Kamati hii na wale wote walioshiriki kwenye kuandika na kutoa hoja na ikiwa na mashahidi mbali mbali ambao Kamati iliwahoji.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii ya Kamati Teule ilianza tarehe 28/01/2014 baada ya Mhe. Ussi Jecha Simai, aliyoitoa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Baada ya hapo sasa tukaazimia kuunda Kamati Teule na tukaahirisha kwa sababu ya Bunge la Katiba, lakini baada ya kurejea kwenye Bunge la Katiba ndiyo kamati ikaanza kazi zake moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kusema kwamba ni ukweli uliopo hivi sasa ni kwamba nyaraka zimeibiwa. Hata tukisemaje; ukweli ni kwamba nyaraka zimeibibwa. Sasa nani kaiba, ilikuwaje, ni hasara gani ni juu ya kamati ambayo kuwa imeleta ripoti na Serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hoja ya kwanza ni kwamba Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ametueleza kwamba nyaraka nyingi zimeibiwa na nchi imeingia hasara kubwa. Lakini nadhani mapungufu yake ni kwamba hatukujua thamani ya hasara ambayo nchi imeipata.

Sasa nadhani ni sehemu ya upungufu wa muda, lakini kamati haikuweza kutwambia kwa nyaraka ambazo zimeibiwa nchi imeingia hasara kiasi gani. Kwa sababu naamini kila nyaraka ina thamani kubwa. Kama mwizi yeye ametumia nyaraka hizi kujinufaisha, itakuwa na nchi imekula hasara kubwa, basi tungekuwa tu ni thamani gani ya fedha ambayo Taifa limeingia kwa wizi huu wa Nyaraka za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba nani wa kulaumiwa kwenye wizi huu. Kwa vyovyote tutakavyosema, kama ni mpenda ukweli wa kulaumiwa ni Serikali yetu ya Zanzibar. Kwa hoja ambazo naomba nizitoe.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, Serikali yenyewe ilikuwa haijui Humoud ni nani, baina ya Zanzibar Serikalini, yaani Wizara na Ofisi ya Mambo ya Nje walikuwa wanagongana; mmoja anasema Humoud ni Ofisa Ubalozi, mmoja anasema Humoud ni Ofisa Mkarabati wa jengo la Beit-el-Ajaib. Kwa hivyo, Serikali yenyewe ilishindwa kumjua ni nani Humoud. Hii nini maana yake.

Maana yake hii ni kwamba watu wanaingia Zanzibar bila ya utaratibu wa kisheria. Ni kuwa Serikali haimjui Humoud nani na alianzaje, wanaamini kwamba ni Ofisa tu anayeshughulikia matengenezo ya jengo mpaka anaathiri nchi Serikali haikumjua. Hilo ni kosa moja Serikali ambalo walitenda na ni lazima wakubali lawama.

Ninashukuru sana Idara ya Mambo ya Nje kwa kutuwekea wazi kwamba Humoud alikuwa ni Ofisa Ubalozi na kwamba hii imedhihirisha kuwa Zanzibar wanaingia watu, kama siafu. Haiwezekani kwamba nchi na watu wanaingia hakuna hata *record* ambayo imeekwa huyu nani na ana madhumuni gani. Kwa hivyo, mwanzo wa kulaumiwa ni Serikali yenyewe kwamba walimuingiza Zanzibar bila ya kumjua nani. Kwa picha hii yeyote anaweza akaingia na akafanya lolote kwa sababu hatumjui nani anayeingia wakati wowote. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini Serikali imekiri kwamba walilijua hili suala kuwa umetokea wizi. Kwa mujibu wa *Hansard* ya tarehe 29/05/2014 ya Mhe. Haroun Ali Suleiman, kwamba Kaimu Waziri amekiri kuwa Serikali ilipata taarifa na ilijua. Na amesema kwenye *Hansard* yake kwamba wahusika waliitwa na wakahojiwa na wakakiri.

Mhe. Waziri, atwambie basi nani aliyewaita, ni hawa Mwanakombo na wenziwe au nani aliyewaita. Ikiwa Serikali iliwaita watu wakahojiwa, wakakiri mpaka Baraza linapiga makelele hakuna hatua, huu ni udhaifu wa pili wa Serikali. (*Makofi*)

Hivyo, mimi nataka Mhe. Waziri aniambie nani aliyewaita; ni hawa watu waliotajwa humu kwenye ripoti ambao wale waliokamatwa watu watatu au yule Humoud na kundi lake ambao ndiyo waliwaita wakahojiwa na kama kuna barua basi ipo barua ambayo iliyoandikwa na Wizara wakaitwa, basi tuletewe barua. Kwa nini hoja yangu hiyo Mhe. Naibu Spika.

Hoja yangu ni hiyo kwa sababu naamini kwamba walioitwa siyo waliokamatwa; Waliokamatwa na Polisi wakatoa uchunguzi, siyo walioitwa na Serikali. Kwa hivyo, walioitwa ni mbali na waliokamatwa ni mbali. Kwa msingi huo walioitwa wanajulikana na ndiyo waliofanya kosa.

Mhe. Naibu Spika, ni aibu kubwa na mimi nataka wale wote walishukiwa wakamatwe naunga mkono watusaidie. Humoud anapowaambiwa kwamba nipeni nyaraka ili na nyinyi mupate pesa kama mabosi

wenu. Mabosi wenu ni wepi? Inaelekea hawa ambao waliopigiwa simu siyo mabosi, kuna mabosi wengine, watwambie ni wepi? Ni Mkurugenzi, ni nani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, nchi imeamua kufufua kaburi na nawaambia mutakuta mengi. Tukiamua kufukua makaburi hapa yatajitokeza mafupa mengi sana ambayo itakuwa ni aibu kwetu sisi kama Serikali.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi siamini kaka yangu pale Mhe. Hamza Hassan Juma, amesema jambo moja muhimu sana. Huyu ambaye Fuad aliyepewa elfu 20, atwambie elfu ishirini ya *Tanzania money, Rial* au Dola. Hatumiani kama yeye anaamini Humoud kwamba atatajirisha, halafu amtoe ofisini mpaka Kiembe Samaki ampe elfu 20, kwanza ni rushwa kwamba amekiri kuwa amepokea rushwa ya elfu 20. Kwa hivyo, sheria ifanye kazi yake kwa mchukua rushwa. Lakini mimi siamini kwamba elfu 20 ndiyo aliyopewa na akaficha ukweli, wakamatwe wote waliohojiwa, waliowasiliana, waliofanya kila hatua ili wasaidie ushahidi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba waliotenda kosa wanajulikana. Ofisi hii ya Mkurugenzi ambaye ametajwa, lakini kuna Omar Sheha kwa mujibu wa Ofisi hii ndiye Ofisa wa Tafsiri ya Lugha (*translator*) na Humoud vereje na nyaraka, yeye alikuja hapa kama mtu anayekarabati majengo, ilikuwaje kuwaje akatoka kwenye majengo mpaka kwenye nyaraka. Twambieni ilikuwaje.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini Serikali walikuwa wanajua na Mhe. Waziri na hasa Mhe. Waziri Haroun atusaidie basi Humoud ilikuwaje kutoka Mambo Msiige kwenye jengo ambaye msimamizi wa ukarabati wa jengo mpaka kwenye Ofisi ya Nyaraka Kilimani, ilikuwaje kuwaje, kaalikwa na kama kaalikwa itakuwepo barua.

Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono kwamba watu wakamatwe, tena kwa nia moja tu, kwa nia ya kutusaidia ushahidi kwamba mabosi waliokuwa wananufaika ni nani. Ni huyu aliyekuweko Marekani ambaye sasa hivi ndiye anayefurahia kwenye *whatssupp* au wengine wapo hapa ndani ya nchi wamejificha. Ninasema hivyo kwa sababu Mhe. Naibu Spika, nina wasi wasi kwamba watakamatwa vidagaa na wataachwa mapapa.

Mhe. Naibu Spika, kama hivyo ndivyo ilivyo, nashauri kwamba Serikali ichukue hatua za kibusara bila ya kuathiri uhusiano wetu na nchi ya Oman, lakini tupate ukweli nani waliohusika. Ni hawa waliokamatwa na kusimamishwa kazi au kuna hawa wakubwa ambao ndiyo walikuwa wakiwatumia wadogo kwa manufaa yao.

Mhe. Naibu Spika, ikifikia hatua hiyo ndiyo nchi itapata ukweli na kwa kweli Wazanzibari watajua nini kilichotokezea.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa watu wamehojiwa, simu zimeonekana hapa kwamba wamepigiwa simu na anaambiwa kwamba "tusaidie ili unufaike kama bwana wako na yeye alivyonufaika", tuambiwe ni nani na wakubwa gani. Sasa wale waliopigiwa simu na wakakamatwa wale ndiyo watatwambia hao mabosi ni wepi.

Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Mkurugenzi alifanya uzembe. Humu tunaambiwa kwamba alikuwa anaumwa na alikuwa hayupo, lakini naamini kwamba wizi huu ilikuwa anaujua na hata kama haujui, wanatwambia kwenye ripoti kwamba Mwanakombo alikuwa anaingia na mkoba na wanamuona, lakini walikuwa wanasubiri ushahidi wa Kinyamwezi.

Kwa hivyo, hii lugha inatutia kizungumkuti kwamba mtu anaiba anaonekana lakini anaachiliwa tu mpaka amalize ndiyo aje aambiwe kaiba, haiwezekani. Ofisi nzima yenye nyaraka ilikuwa ina tatizo na naamini

kwamba viongozi wa Ofisi ya Nyaraka ndiyo tatizo, wakamatwe, wahojiwe watusaidie badala ya kuwakamata watu ambao nadhani watakuwa hawana mchango mkubwa kwenye kutoa majibu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hoja hizo, nasema kwamba Serikali iwe makini ili kulinda uhusiano wetu sisi Zanzibar na Oman, lakini wale magwegwe waliofanya makosa haya badala ya kuonea wadogo wakamatwe, watafutwe. Ninaamini mukimkamata Humoud, hii leo Humoud mukimkamata atasema nani aliyekuwa akimsaidia kupata taarifa hizi.

Mimi siamini kwamba mtu atakuwa mpumbavu kiasi hicho. Humoud leo mukimkamata atawaambiwa kule aliingiaje, alianzaje na huyo bosi aliyemnufaisha ni nani; ni wale wadogo wadogo wenye mkoba wanaosukana au nani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa jinsi ya upeo wangu ninavyoamini, wale wanaosukana ni chambo tu, lakini kuna watu ambao walikuwa wananufaika na nyaraka hizi na ndiyo chanzo. Hawa waliokamatwa wote nina hakika hawajui Kiingereza wala Kiarabu, mpaka aamini kwamba hii nyaraka ina maana; nyaraka ya Kiingereza au Kiarabu ataijuaje Hija. Kwa hivyo, anayeijua thamani ya nyaraka ni yule mwenye kujua kitu ambacho kimeandikwa.

Kwa hivyo, wale waliokuwa wakisukana nadhani walikuwa wanatumikia mabwana. Sasa nadhani wakamatwe wote kwa ujumla wahojiwe ili tuwajue na mwanzo wa kukamatwa naungana na Mhe.Hamza, kuwa wa kukamatwa mwanzo ni Humoud atwambie kule alifikaje ili tupate ukweli na tuweze kuisaidia Serikali.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja na mapendekezo ya kamati.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Hija. Sasa nafasi ni ya Mhe. Mohamed Haji Khalid, baadae Mhe. Wanu Hafidh Ameir na ajiandae Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kutoa machache sana juu ya kadhia hii iliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha Jumamosi ya leo kuwa ni siku ya kazi kinyume na utaratibu wa kawaida. Pia, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kuwasilisha kwake ripoti hii kwa umakini sana. Mhe.Naibu Spika, mimi nilikuwa ni mjumbe wa kamati hii. Kwa hivyo, niwapongeze watu wa nyaraka; watu wote wale ambao tulishirikiana nao katika kufanya kazi hii muhimu na ngumu.

Pia, nimshukuru Mhe. Abdalla Mohamed Ali, ambaye yeye tulimchukua kama ni mtaalamu wa lugha ya Kiarabu na kama mtu alitokea wakati alipokimwaga Kiarabu angelidhani kuwa huyu ni Mmanga kutoka Oman, kumbe ni Mmanga kutoka Makombeni. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu kuhusu mazingira ya lile jengo binafsi. Nadhani ofisi ile ilipoanzishwa mwaka 1963, mazingira yake hayakuwa kama yalivyo leo. Ninadhani ilikuwa ni pahala jengo lipo peke yake, ilikuwa halikuzungukwa na nyumba nyengine za kibinafsi. Lakini leo jengo lile limezungukwa na mlango wake mkuu pia ni mlango wa nyumba ya mtu binafsi.

Lile ni moja katika tatizo kubwa, gumu na sugu. Hata tukiweka mlinzi mwenye mzinga, kwa sababu lango kubwa la kuingilia pia ni lango ni kuingilia la mtu ya nyumba ya mtu binafsi; hatuwezi kumzuiwa mtu binafsi kuingia katika nyumba yake. Kwa hivyo, Serikali ifanye jambo moja, imtafutie mmiliki wa

nyumba ile pahala ama wamjengee au wampe pesa za kutosha za kuweza kujenga nyumba nyengine, pale aondoke ili eneo lote lile, liwe ni mazingira ya jengo lile letu la nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, upotevu wa nyaraka hizi ni sehemu ya kuipoteza historia ya Zanzibar. Kwa sababu nyaraka nyingi zilizopotea zinahusu mambo ya tawala za kifalme zilizopita miaka kama 150 nyuma.

Mhe. Naibu Spika, kuna nyaraka ambazo wafalme walikuwa wanafanya mahusiano na nchi nyengine. Nyaraka hizi zimepotea. Kuna waraka ambao ulipiga marufuku biashara ya utumwa, waraka huu haupo. Kuna waraka ambao ulikuwepo kwa ajili ya utumwa Zanzibar, waraka ule kadhalika nao haupo. Hii ina maana nyaraka nyingi zilizochukuliwa ni kujaribu kuondoa historia halisi ya Zanzibar.

Hili ni jambo la kawaida kwa Zanzibar kwa sababu hata sisi tuliopo leo, kuna sehemu ya historia yetu tunaipotosha na tunaikataa. Kwa mfano sisi tuliopo leo tunaokataa uhuru wa mwaka 1963. Tunapoandika historia ya Zanzibar kwa wananchi leo, uhuru wa mwaka 1963 hautiwi hesabu kuwa ni uhuru, ni kupotosha historia hata uwe na siku moja, mbili au tatu, lakini ulikuwa ni uhuru. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini katika historia yetu uhuru huu hautiwi wa hesabuni. Kwa hivyo, tuna tabia ya kujaribu sisi Wazanzibari wenyewe kupotosha historia yetu. Kwa hivyo, lengo kubwa na upotevu huu ni kupoteza historia halisi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nyaraka nyengine zilizopotea ambazo mule hazimo ni nyaraka za majengo ambayo ni majengo makubwa na muhimu sana leo katika nchi hii, ni majengo, waraka wake haupo. Sasa hata kama majengo hayo pengine iwe yametaifishwa, lakini utaifishaji wake ulikuwa *verbal* na hiyo sauti ya kutaifishwa ilihifadhiwa au ilikuwa ni kwa maandishi. Kama hakuna, huyo aliyechukua waraka huu iko siku kuna bahali pakubwa sana atakujapadai na atakuwa na haki hiyo kwa sababu waraka wake anao.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki niseme nani kaiba na kapeleka wapi, lakini niseme nyaraka zimepotea tena nyingi sana, tena zile ambazo ni muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, kuna vitabu ambavyo ni vya tiba havipo na vile vichache vilivyobakia vimeshataabanika. Kuna vitabu tulipojaribu kuvifungua kurasa zake zinagandana. Ninachoshauri kwamba taasisi hii ifanye maarifa ya kuvihifadhi vitabu vile ili virudi katika uhalisia wake, vyenginevyo, hatimae vitageuka unga wa karatasi.

Mhe. Naibu Spika, halikuibiwa buku zima la nyaraka kama ilivyo, lakini watu wanapoazima pengine kwenye kurejesha. Kwa sababu hakuna uangalifu wa *page* baada ya *page* kuna vyengine kuna *pages* fulani tu zimechukuliwa katika kitabu fulani kilichoazimwa. Wengine ni wataalam hawakuchukua *the whole volume*, lakini kachukua kitabu katazama kaona sehemu hii naihitaji akatoa ukurasa. Katika upekuzi wetu tuligundua kuwa kuna baadhi ya vitabu vimenyofuliwa. Vimerudishwa lakini baadhi ya kurasa hazimo.

Kwa kweli *system* ya uwazimaji na urejeshaji si mzuri, tulibaini kuwa yule anayeazimisha anaandika sehemu ya yule aliyempa kitabu. Kwa hivyo, inaonekana yule anayetoa kitabu ndiye anayechukua kitabu. Yule anayetoa waraka inaonesha yeye ndiye aliyechukua ule waraka. Sijui inawezekana kwa taaluma nyengine hiko hivyo, lakini katika hali ya kawaida ya uwekaji wa kumbukumbu unaona kuwa ile ni kasoro, pengine ni ukosefu wa lugha kama nilivyokuwa mkosefu mimi wa lugha ya Kiingereza.

Mhe. Naibu Spika, tatizo hilo lilikuwa lipo, kwa hivyo, ili kuondoa kasoro hizi ndogo ndogo, taasisi ile wafanyakazi wake wapewa mafunzo ya kuweza kutunza na kuweka kumbukumbu sahihi.

Mhe. Naibu Spika, pia, kulikuwa na mgongano baina ya Kamisheni ya Wakfu na hii taasisi. Kuna nyaraka taasisi imedau kuwa tumewaazima watu wa Kamisheni na zipo ambazo walizokubali kuwa ni kweli wamechukua na zipo walizokataa kwamba hawakuchukua, lakini sisi wametwambia kuwa wamewapa watu wa Kamisheni. Kwa hivyo, taasisi mbili hizi na watu wa Kamisheni wanashughulika na sehemu fulani tu sio kila kitu, lakini tumekuta kuna mgongano wa aina hiyo. Ili kuondoa migongano ya aina hiyo, lazima taaluma ya kuchukua na kurejesha nyaraka ielezwe na iwe nzuri zaidi. Vyenginevyo, Mhe. Naibu Spika, historia na rasilimali yetu itatupokea bila ya kujua.

Mhe. Naibu Spika, mchangiaji mmoja hapa kasema kuna watu wanadhani kuwa waraka si karatasi tu. Nyaraka hizi ni karatasi lakini si karatasi tu. Ni kweli ni karatasi lakini ni karatasi zenye thamani tena kubwa. Kwa sababu hao wanaozitafuta sio wapungumbavu kuwa watafute nyaraka hizi kwa pesa nyingi halafu ziwe hazina thamani. Zina thamani na zina umuhimu wake, nyengine ni za umiliki wa mali zilizokuwemo ndani ya Zanzibar, nyengine ni historia ya Zanzibar, yengine ni kumbukumbu muhimu za Zanzibar. Serikali ilichukuwa juhudi ya kukusanya kumbukumbu zile kwa pamoja ili zitumike leo, kesho, keshakutwa na muda mwengine wowote hadi mwisho wa dunia. Lakini kila siku zinachukuliwa kidogo kidogo.

Mhe. Naibu Spika, upetevu huu haukuwanza pale tulipoona sisi tu, umeanza miaka mingi nyuma. Tatizo la Serikali pale anapobainiwa mtu fulani kafanya uhalifu fulani hukumu yake kubwa yaani adhabu kubwa anayopigwa ni *transfer*.

Mhe. Naibu Spika, uhamisho si adabu wala sio adhabu uhamisho ni jambo la kwawaida kwa mtumishi wa Serikali.

Mimi nilikuwa mwalimu zamani na mkataba wangu niliofungishwa ulikuwa kwamba utafanyakazi katika sehemu yoyote ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa hivyo, ningepigwa uhamisho kutoka Kengeja nikapelekwa Makunduchi ingelikuwa sio adhabu, kwa sababu ni mkataba wa kazi. Ningepelekwa Kisiwa Panza hata kama wakubwa wangu wawe wamefanya kwa adhabu, mimi mwenyewe ningeona kuwa sio adhabu kwa sababu ndio mkataba niliosaini wa kazi kwamba nifanye kazi popote ndani ya Zanzibar.

Kwa hivyo, leo mtu kafanya afanyavyo unamtoa pale unampeleka pengine, unasema ndio unamtia adabu. Sijui adadu ya Serikali hii ikoje, kuwa uhamisho ni adabu, ina maana nchi hii haina uhamisho. Kwa hivyo, watu wafanye wafanyavyo hata wakishakushiba wahamishwe na wapelekwe pengine wakachume upya.

Mhe. Naibu Spika, kadhia hii lazima itafutwe nani kahusika na anayehusika hatua za kisheria dhidi yake zichukuliwe. Kama kweli Serikali ina ithamini na inakubali kuwa kumbukumbu iliyokuwepo pale ni mali Taifa, basi lazima hatua zichukuliwe na namna bora ya kuzitunza iimarishwe. Haitakuwa vyema kabisa kuwa tumetumia wiki sita, kufanya kazi ile ngumu, kutokana na mazingira ya mule sisi wengine tulivyorudi tunakohowa kama paka. Halafu Serikali iyone kuwa ripoti imeletwa, watu washasema wasemavyo na lende lendako. Hii Mhe. Naibu Spika, itakuwa Baraza hili halifanyiwi haki na Serikali. Serikali imetuma Baraza, Serikali tunaipa ripoti yetu, Serikali lazima ichukuwe hatua muafaka, tusimuonee mtu lakini pia isimpendelee mtu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitashangaa kweli kweli, kuona kuwa Serikali kuhusu kadhia hii ya upotevu wa nyaraka kama itakaa kimya kama iliyokuwa na baridi. Kwa sababu mtu akiona baridi huchukua blangeti akajivunga vunga akawa anatetemea. Je, Serikali kuhusu suala hili itajivunga blangeti ikae kimya. Kama itakaa kimya kama ilivyokaa kwenye Kamati nyengine, nitapendekeza kwenye Baraza lijalo baada ya uchaguzi kuwa Kamati Teule zisiundwe tena. Itakuwa hazina maana, mpaka ripoti hii ya Kamati Teule tujuwe matokeo yake, hakuna hatua hasa zilizochukuliwa dhibi ya wale wambao wamezikhalifu sheria.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kuwa nilikuwa mwana Kamati sina mengi ya kusema, lakini kama nilivyoanzia nataka nimalizie mazingira ya ile ofisi sio nzuri kwa sababu ina langu kuu na mlango wa mtu binafsi. Lile ni moja katika tatizo mama, huwezi Ofisi kubwa kama ile ya Serikali ikawa mlango wake wanatumia na watu wengine ambao hawamo katika ile taasisim, hata tuweke mtu mwenye mizinga mikubwa namna gani, huwezi kumzuia mtu kuingia katika nyumba yake kwa sabaubu una mzinga tu. Vyenginevyo, tutatute njia yoyote ile inayowezekana lakini lango lile litumike kwa ile Ofisi tu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba naiyumba mkono mia kwa mia ripoti hii ningeomba Serikali baadae itafakari na ichukue hatua za kufaa dhidi ya wote wale watakaohusika kuwa na makosa kwenye kadhia hii. Ahsante sana.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie katika ripoti hii ya Kamati Teule ya Baraza ya kuchunguza upotevu wa nyaraka katika Jengo la Nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kwa kuanzia naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukutana hapa leo ili kuendelea na shughuli zetu za Baraza. Lakini pili nikushukuru wewe kwa nafasi hii ya kunipa mimi kuchangia ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuchangia naomba nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wangu wa Kamati kwa uwasilishaji wake mzuri, lakini pia nimpongeze kwa uwongozi wake katika muda wote ambao tulikuwa naye ametuongoza vizuri hadi jana kuwasilisha ripoti hii ya Kamati.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ripoti imeshaeleza na mimi kama Mjumbe wa Kamati hii sitokuwa na mengi sana ya kueleza, mengi yameshaelezwa kwenye ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuanza kuchangia ripoti hii naomba kwanza nitoe masikitiko yangu kwa Baraza. Tunapounda Kamati Teule kwa maana ya kwamba tunatakiwa kuiwezesha Kamati Teule ile kufanya kazi kwa namna moja au nyengine ili kuona kwamba inafanya kazi zake kwa ufanisi. Nasema haya ripoti imeelezea kwamba muda, nyenzo na kila kitu ambacho ilitakiwa Kamati ile ipate haikupata vizuri.

Mhe. Naibu Spika, tunapounda Kamati Teule tusiangalie tu kwamba kiasi gani hawa Wajumbe wanakwenda kupata, tuangalie kiasi gani wanakwenda kufanya kazi huko na kuileta hapa. Kama mnavyoona muda tuliopewa ni mfupi na muda wenyewe kwanza tulipewa siku saba, siku saba tumekaa hatukufanya chochote ilibidi turudi kwa Spika, kushajihishana tuombe muda mwengine. Tukapewa wiki mbili, wiki mbili tukaenda wiki moja na nusu yote tumemaliza kwenye Ofisi ya Nyaraka kutizama yale maboksi.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru nimepata *experience* ya kutosha katika chumba kile kiasi ya kwamba hii leo ukinifungia ndani mule nusu ya maboksi yale kwa muda mfupi nitakuwa nimeshayapitia yote, maana nimejua kuanzia zile *index* na kila kitu. Nashukuru kwamba nimejifunza mambo mengi, nimegundua kwamba zamani kulikuwa kuna ziwa linaitwa "*river one"*.

Mhe. Naibu Spika, nimejifunza mengi katika Ofisi ile. *Point* yangu ni kwamba tunapounda hizi Kamati Teule basi tuziwezeshe kufanya kazi zake, usiangalie kiasi gani wajumbe wale watapata, lakini angalia ile *quality* ya kazi ambayo watakwenda kuifanya huko na kuileta hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri Wajumbe wote wameridhika na ripoti hii, pamoja na kuwa tumepewa wiki sita, lakini watu wameridhika na ripoti hii ambayo imeletwa. *At least* imeonyesha ile picha halisi ya mambo ambayo yanatokea kule.

Mhe. Naibu Spika, nyaraka nyingi zimepotea na kama Kamati ilivyopendekeza kwamba kuna vyombo vyengine vinaendelea na uchunguzi, tunaomba viendelee na uchunguzi huo na hatua kama Mhe. Hamza, alivyosema hatua za kisheria zichukuliwe dhiti ya wale wote ambao watagundulikana. Pamoja na kwamba anasema ripoti haijasema lakini kama watu wazima, ripoti kama hii Serikali haiwezi ikawafumbia macho hivi hivi, tutawashangaa sana. Kwamba mambo haya yote yaliyoelezwa humu halafu Serikali ikae kimya tu, ije hapa na iseme maana yake ooh, mtendaji kaondoshwa na kapelekwa sehemu nyengine ndiyo adhabu aliyoipata.

Tunasema hivi kwa sababu hii ndio *practice* ya Serikali kila siku. Mambo yanakuja hapa badala yake mtendaji anaondoshwa kwenye shirika au kwenye ile nafasi anapelekwa sehemu nyengine hiyo ni *bad practice,* waacha. Tukisema watu wachukuliwe hatua, watu wachukuliwe hatua ili watu warudishe imani na Serikali hii, mshasemwa sana, hebu *act on this, at least on this one act.* Chukuweni hatua tuone kwamba kweli Serikali imechukua hatua juu ya hili jambo.

Mhe. Naibu Spika, jengine Kamati wakati inafanyakazi zake ilishauri sana na wale wataalam wa mambo ya nyaraka, kwamba hetu ombeni mtoke kidogo, mwende kwenye nchi za wenzenu mkaone jinsi gani watu wanahifadhi hizi nyaraka. Na hawakututajia mbali kwa sababu walijua mambo haya, wakasema angalau nendeni hapo Nairobi mkatizame.

Mhe. Naibu Spika, watu wameweka breki za mbuzi. Tumeomba na kuomba hakuna lolote lililokuwa na sio kwamba tulikuwa tunakwenda kwenye *tours* tu au kwenye *picnic* kwenda kutizama. Tulikuwa tunakwenda kutizama yale mambo mazuri ambayo wenzatu wanafanya ili na sisi tulete huku kwetu tuone ni jinsi gani tunavibakisha hivyo vinyaraka vilivyobaki, maana nyingi zimeenda kuna vinyaraka tu ambavyo vimebaki, zile nyaraka za maana nyingi hazipo.

Mhe. Naibu Spika, ninalosema kwamba tunapounda Kamati hizi Teule basi tuwe tayari kuziwezesha Kamati hizi kufanya kazi zake vizuri.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nichangie kidogo kwenye hii ripoti ya kamati yenyewe. Kwa kuanzia Mhe. Naibu Spika, naunga mkono mapendekezo ya Mhe. Hamza pamoja na kwamba amesema kwamba hayakuandikwa katika ripoti yenyewe lakini sisi watu wazima tuna-*expect* kuwa huwezi ukaja na mambo haya yote halafu kusichukuliwe hatua.

Kwa hivyo, pamoja na kwamba hatukuandika lakini tunaamini kwamba Serikali itachukua hatua juu ya wale wote waliohusika katika kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, katika hili naomba niseme "tusi-*deal* na vidagaa tukaacha mapapa"; hawa wengine waliotajwa sijui kina Mwanakombo na wenzake kama yeye Mwanahawa hata yeye hahusiki mazingira tu ndio yamtia katika mkumbo. Lakini kuna wengine ambao hawahusiki na hapa Mhe. Mohammed amesema kwamba wanawake tunakuwa waaminifu sana, lakini sasa anasema sasa kwamba wanawake wa Baraza hili inabidi twende tukawafunze wale, haina haja ya kuwafunza.

Wale wasingeyafanya waliyoyafanya kama sio *bad influence* waliyoipata kutoka kwa wanaume, wanaume ndio waliowashawishi na wakafanya yale. Sisi bado tunaendelea kuamini kwamba sisi wanawake waaminifu na waadilifu, lakini mazingira ambayo yamewekwa kati na Mhe. Naibu Spika, sitaki kusema mengi lakini kulikuwa, pia kulikuwa na mahusiano fulani baina huyu mwanamke mmoja na kiongozi wa taasisi hii. Kwa hivyo. ndio maana haya ninahisi yakapelekea pia na ule ushawishi ukawa mkubwa zaidi juu ya kuiba hizi nyaraka.

Sasa Mhe. Naibu Spika, wakati wa mahojiano wapo waliokataa na wapo waliosema kwamba wao hawahusiki, hawajaiba akiwemo kiongozi mkuu wa taasisi hii. Lakini niseme tu kwamba uzembe ambao

uliofanyika pale *fine* sisi tumeamini hajaiba, lakini uzembe ambao uliofanyika pale unatosha kabisa kumtia hatiani na mamlaka yanayohusika yakamchukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, *negligence* na *recklessness* mpaka Mahakamani huachwi, lazima utatiwa kwenye hatia. Sasa tutashangaa sana kama Serikali italifumbia macho hili na kuacha watu waendelee kufanya wanayofanya.

Mhe. Naibu Spika, tushaibiwa vya kutosha, hii iwe adabu sasa na huu haujaanza hapa, waswahili wanasema tu "za mwizi arubaini", arubaini sasa imefika na tunaamini kwamba Serikali itatoa dawa kwa wale ambao wote wamehusika katika kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, umaskini wetu usitufanye kwamba tukachezewa tunavyotaka, kweli maskini tuna njaa, lakini haiwezekani kwamba *just because* nchi inatusaidia. Kwa hivyo, ije hapa ifanye inavyotaka. Wakae na utajiri wao wacha sisi tufe na njaa zetu lakini nyaraka zetu ziwe *safe.*

Sitaki kukugusi huko kukubwa lakini najua Serikali itachukua hatua kwa mujibu watakavyoona wenyewe na hatua ambazo zitaturidhisha sisi sote. Lakini hili si jambo la kufumbiwa hawezi mtu akaja kwenye nyumba yako akafanya anavyotaka, wageni kawaida huishia ukumbini huyu kaingia mpaka chumbani. Tena pale anayajua majina ya kila mmoja, yaani ile Ofisi ya Nyaraka anaijua *in and out, free* akienda akiambiwa andika jina, kuna utaratibu unaandika anasema mimi *diplomatic,* haandiki jina na hao hao wafanyakazi wametwambia kwamba, anaingia kule *strong room* anavyotaka saa nyengine anakuwa na mtu ambaye anahusika pale.

Lakini pia ana uhuru mkubwa wa kufanya chochote pale anachotaka. Na mbaya zaidi anawadanganya hawa na *gift*, yaani mimi nimesoma historia sitaki kusema mengi, yale mambo yaliyokuwa yanafanyika enzi zile yaani kama yamejirudia; kama vitambaa, tende, vi-*gift gift* vidogo vidogo vile wanavyopewa wafanyakazi watu wanapenyeza nyaraka, ni njaa.

Kwa hili Mhe. Naibu Spika, Serikali ione kwamba wajaribu kwa namna watakavyoweza kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa pale kama ripoti ilivyoeleza, kwa sababu inaonekana hali iliyopo, nyaraka ilikuwa ina hali mbaya. Kabla ya haya kutokea imetengenezwa juzi tu, nafikiri muda mfupi baada ya haya kuanza kusemwa semwa ndio kumetengenezwa, kumewekwa *CCTV camera* na *carpet*.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka katika bajeti moja Mheshimiwa Mjumbe mwenzangu wa Kamati ya Katiba na Sheria alisema. Viti vimefungwa kamba ya katani pale Nyaraka, *carpet* chini kama chumba cha msela, yaani ilikuwa husemi kama hii Ofisi ya Serikali, baada ya kutokea haya ndio kumebadilishwa badilishwa kidogo angalau kunatizamika. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hili nalo pia Serikali walione.

Sasa Mhe. Naibu Spika, sitaki kumaliza pumzi haya ya kawaida tu tunasema halafu ngoma inakuja pale pale *nothing*. Kwa hivyo, sitaki kumaliza pumzi naomba niishie hapa, tumesema vya kutosha. Ripoti zimekuja tumesema na hii imekuja tunasema na naamini wajumbe wengine watasimama watasema, kazi yetu sisi tutabwatuka halafu hakuna kinachoenda.

Lakini tumesema vya kutosha Mhe. Makamu wa Pili amesikia, Serikali kwa ujumla imesikia na naamini kama Mhe. Rais hajasikia lakini taarifa atazipata. Kwa hivyo, tunaomba katika hili, hebu chukueni hatua angalau hawa wengine waogope, kwa sababu kama hakutofanywa chochote watu wengine naamini sio Humoud tu peke yake anayetaka hizi nyaraka wako wengine tele, hapa watu wanakuja na nyaraka zao *original* kabisa mtu anasema mji wa Chake Chake wote wake kumbe nyaraka zimetoka pale pale kwetu, zinaibiwa pale wanapenyezewa mtu anaenda huko anakaa akirudia anasema Wete nzima yangu, Chake Chake, nzima yangu na nyaraka zinatoka pale pale.

Kwa hivyo, Serikali tunaiomba ilifanyie kazi hili waliohusika wote wachukuliwe hatua na narudia tena "msiwaonee vidagaa mkawaacha mapapa". Hatua zichukuliwe kwa wote waliohusika ili angalau hivyo vinyaraka vilivyobaki vinusurike.

Baada ya kusema hayo naunga mkono ripoti hii asilimia mia na naomba wajumbe waliobaki nao wachangie na kuunga mkono na naomba Serikali iyachukulie yale yote ambayo yaliyosemwa katika ripoti hii kwa uzito wake na hatua zichukuliwe hatua ambazo zitaturidhisha sote, sio ya kumhamisha mtu hapa na ukampeleka pale.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mawazo yangu mawili matatu yanayohusu kadhia hii ya upotevu wa nyaraka muhimu za nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nataka niipongeze sana kamati kwamba pamoja na muda mdogo sana waliopewa kufanya kazi tena kazi nyeti kama hii kazi ya kitaalamu sana, lakini wameweza kugundua mambo mengi na hatimaye wametutayarishia ripoti hii na wametuletea ili kuonyesha yale mazingira hasa yalivyokuwa. Kabla sijaendelea kwanza niikubali kabisa hii ripoti ya kamati, ninaiunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika, kadhia hii ya nyaraka ilikuwa kwanza ikizungumzwa kisiri siri ilipoanza kutokea kwanza tulikuwa tunasikia sikia tu kisiri siri baadae katika ripoti yetu ya Kamati ya Katiba na Sheria tukaileta hapa Barazani na Mwenyekiti wetu Mhe. Ussi ndie aliyetoa wazo la kuunda Kamati Teule ili kwenda kuchunguza. Sasa kamati imekwenda imechunguza na kwa bahati walipofika pale tayari ile taasisi yenyewe ya nyaraka imeshachukua baadhi ya hatua, nimeona humu kiambatanisho kimoja Mkurugenzi anaiarifu Polisi ije ifanye uchunguzi kabla ya Kamati Teule haijaundwa. Kwa hivyo, na yeye alishtukia na akaanza kuchukua hatua zake. Sasa Baraza kama wajibu wake wa kusimamia Serikali nalo limeunda Kamati Teule kwenda kuchunguza ni jambo jema sana.

Lakini kadhia zote hizi Mhe. Naibu Spika, zimewa-*accused* watu watatu zaidi. Watu waliotuhumiwa moja kwa moja kwanza ni Mwanakombo Ali, huyu Mwanakombo huyu katajwa dhamana yake pale yeye ndie mtunza chumba cha nyaraka. Mtu wa pili ni Mwanahawa ambaye yeye ni mfagiaji na mtu wa tatu aliye-*accused* ni Humoud ambaye anafanya kazi katika Ofisi ya Ubalozi mdogo wa Oman ulioko Zanzibar.

Sasa mimi nasema kwa sababu angalau tuna pa kuanzia basi hawa kwanza wachunguzwe na ikithibitika basi waadhibiwe kwa mujibu wa sheria. Ila katika hili Mhe. Naibu Spika, nilikuwa napenda nitoe tahadhari moja, Zanzibar na Oman ina uhusiano mzuri sana tena wa zamani, Waoman walitutawala hapa Zanzibar, wakafanya mambo mengi, baada ya muda wakaondoka tukawa tumejitawala wenyewe.

Lakini kuondoka kwao hakukuleta uhasama mkubwa katika nchi. Na kinachoendelea nini, kinachoendelea sasa hivi ukenda Oman Wazanzibari wako kwa magunia na hapa Zanzibar Waoman wapo kwa magunia tunatembeleana. Na hata *direct route* ya ndege kutoka Oman kuja Zanzibar kila baada ya siku mbili inatua hapa, inachukua Wazanzibari waliomaliza istikama zao kule inawaleta huku na inachukua Waoman inapeleka kule, ndio kazi inayofanyika uhusiano mzuri.

Sasa nilikuwa naomba sana katika kulishughulikia hili basi tuzingatie pia uhusiano uliopo kati ya nchi hizi mbili. Humoud kafanya kosa kuwashawishi wafanyakazi wa taasisi wa nyaraka kuiba nyaraka na kumuuzia, lakini aliyefanya kosa ni Humoud. Naomba akipatikana na hatia ahukumiwe kama Humoud, isije ikahukumiwa nchi kwa kosa la Humoud. Na naomba sana Serikali ifanye *negotiation* ya ziada na

nchi ya Oman ili nchi ipate kujisafisha au iseme wazi kama Humoud walimtuma au Humoud ni *incentives* zake mwenyewe, tusije tukafanya uhusiano ukalega lega kuna matatizo makubwa yanaweza yakatokea. Hilo moja Mhe. Naibu Spika, nilitaka niliseme kama tahadhari. Kwa sababu uhusiano wa nchi na nchi jambo muhimu sana na una faida kubwa.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana uchunguzi uendelee kufanyika kwa sababu walichokifanya kamati na kwa sababu hawakuwa na muda wa kutosha wao walifanya *sampling.* Kwa mfano boksi la kwanza ambalo lilikuwa na nyaraka 150 waligundua 2 zimetoweka, boksi la pili lenye nyaraka 30 nyaraka 9 hazimo, boksi la tatu lina nyaraka 55 nyaraka 10 hazimo, boksi la nne nyaraka 27 nyaraka 5 hazimo. Boksi jengine lenye nyaraka 139 nyaraka 12 hazimo, maboksi kama 9, 10 waliyafanyia ukaguzi. *Of course,* hawakuweza kuyafanyia ukaguzi yote kwa sababu hayakuwa na muda wa kutosha.

Lakini kama tukipata muda wa kutosha, basi tutagundua nyaraka nyingi zaidi zimepotea na zimepotea kwa nyakati tofauti, pengine nyengine hizi zimepotea kabla ya uhai wa Humoud kuwepo, kwa hivyo, inawezekana ni watu wengine kabisa waliohusika huo uchunguzi ufanywe ili ugundue mambo kama haya.

Sasa kwa sababu nyaraka zetu zimepotea nyingi na kwa mnasaba huu inawezekana nyingi zinaelekea Oman, sijui huyu Humoud kule anaziuza au anazipeleka Serikalini, sijui lakini zinaelekea huko. Sasa nilikuwa naomba sana Serikali jambo jengine ambalo ni muhimu kulifanya ni kuwasiliana na Serikali ya Oman ili Serikali ya Oman isaidie kuzitafuta hizi nyaraka zilizopotea na zirejeshwe Zanzibar.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo niliunganishe hapa hapa kwa mujibu wa taarifa nilizonazo ni kwamba kulikuwa na mazungumzo yakifanyika kati ya Serikali ya Oman na Serikali ya Zanzibar kuhusu kuandaa mkataba wa makubaliano ili nyaraka hizi labda kama wapewe kule au kama kutafunguliwa kitengo kule Oman au kama wanapewa au vyenginevyo vyovyote, lakini kulikuwa kuna mazungumzo hayo.

Sasa nilikuwa nafikiria kuishauri Serikali kwamba haya mazungumzo basi bora yangeendelea na yatakapoendelea mpaka yakafika pahali pazuri pia itakuwa njia nyepesi ya kuzipata zile nyaraka zetu ambazo zimekwenda kule kinyume na utaratibu. Kwa hivyo, hilo nilikuwa naomba sana Serikali ilizingatie.

Jambo jengine na la mwisho ambalo nilitaka niliseme ni lile alilolisema mwenzangu Mhe. Wanu. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na miongoni mwa taasisi ambazo tunazikagua ni taasisi hii ya Nyaraka. Na ripoti yetu ya mwaka jana tulisema kwamba Serikali iliitelekeza Taasisi ya Nyaraka, mazingira yake ni machafu, haina vifaa hata humo zinamokaa hizo nyaraka wewe ukenda mle huwezi kukaa hata dakika tatu unaweza ukapata mafua harufu mbaya.

Hawana vifaa vya kisasa vya kuweza kuhifadhia nyaraka, pale pahali penyewe haparidhishi hapana usalama wa kutosha. Kuna nyumba pale tumepiga makele wee nyumba ya mtu binafsi imo ndani ya eneo la majengo yale ya nyaraka, tumepiga makelele kweli kweli, sijui yule anayeishi mule ni mfalme gani hata anashindwa kuondoka mle. Na kama haondoki, kwa nini Ofisi ya Nyaraka haihami ikahamia pahali pengine penye usalama zaidi, tumeyasema humu.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ile haina gari hata ya Mkurugenzi, kwa masikitiko makubwa Mkurugenzi akitaka kufanya safari zake za kikazi anaomba gari kutoka Idara nyengine yeye hana, hamna samani mule, tumekwenda *Wallahi* yuko Mzungu anafanya *research* kakaa kwenye kiti, hicho kiti kimefungwa kamba ya mkonge, utafikiri kiti cha kuingia kule shamba kwa wale waliokuwa wanainga inga shamba za mipunga. Sasa Serikali imeitelekeza hii Ofisi, ni rahisi mtu kuweza kupenya penya.

Jambo jengine walioko mule hawana taaluma wala hawajui thamani ya nyaraka, maana mtu kama anajua thamani ya nyaraka, kwa nini atoe nyaraka kwa shilingi 20,000. Sasa kwa kifupi na Serikali nayo hapa ina tatizo. Nyaraka ni kitu muhimu sana ina mambo mengi sana ya historia ya nchi, ni sehemu ya mapato ya nchi, ni sehemu ambayo ikitunzwa vizuri inaweza kusaidia matatizo mengi ambayo yanatokea katika nchi. Leo tunaiweka kama mtoto wa kambu.

Mhe. Naibu Spika, tumesema na tutaendelea kusema, kwa nini hawatafutiwi jengo madhubuti wakatafutiwa vifaa kwa sababu nyaraka nyengine mule kuna hoja moja nimekuta humu wanasema Mkurugenzi aliwazuia watu wasiendelee kuzipekuwa pekuwa kwa sababu zinamung'unyuka,zikimung'unyuka unaweza kukosa hata kumbukumbu baadae. Kuna vifaa maalum vya kuweza kuzi-*renew* na kuziweka zile katika hali ya usalama zaidi, vifaa hivyo havipo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani tukubalini kwamba wizi umetokea, walioiba wamefanya makosa ya jinai wachukuliwe hatua, lakini na Serikali kuazia sasa hebu tuone kama tuna jambo la kujifunza. Tuishughulikie ile ofisi kama ni *strong room* iwe ni *strong room* kweli kweli iwe na mlinzi na huyo mlinzi awe mtaalamu anayejua thamani ya nyaraka, tuone kama na hizi nyaraka zitapotea tena. Kwa hiyo, naomba mambo yote yachukuliwe hatua kwa mujibu ya mazingira yalivyo.

Mhe. Naibu Spika, nilisema awali kuwa naunga mkono hii na naendelea kusema tena kuwa naiunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana.

**Mhe. Omar Ali Shekhe:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika jambo hili muhimu sana, sana katika uhai wa Taifa letu. Baada ya kukushukuru wewe niipongeze Kamati hii Teule ambayo binafsi nakiri kwamba imefanya kazi kubwa na kazi yakupigiwa mfano. Lakini kama wenzangu walivyotangulia kueleza na mimi nieleze masikitiko yangu ya mazingira magumu ambayo kamati wamefanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba ripoti hii hasa haikukamilika, ripoti haijakamilika bado kwa sababu kukamilika kwa ripoti tulitaka angalau wafike pahala, kwa sababu leo tunaambiwa ni Humoud ni diplomasia na kwa sababu huyu alikuwa ni mwanadiplomasia, kuna namna mbili inayojitokeza hapa; Namna walivyotumwa na nchi yake kufanya alivyofanya au kukanushwa kwa nchi yake kwamba yeye alifanya kama Humoud, hakufanya kama ni mwanadiplomasia.

Mhe. Naibu Spika, sasa hapa pana kitendawili hapa suala hili tutali-*treat* vipi. Kwa hivyo, kwa vyovyote vile kamati walau ilikuwa ituoneshe njia katika hilo, maana yake ni kwamba kwa vyovyote kamati wangalilazimika kusafiri na kwenda katika nchi iliyohusika katika Balozi iliyohusika na kupata chochote kinachohusiana na suala hili. Leo hili huwezi ukalihusisha, unaweza ukamuhusisha Humoud kama Humoud, lakini huwezi hata siku moja Mhe. Naibu Spika. Huwezi hata siku moja ukaikwepesha *Embassy* ya Oman katika suala hili na hasa kwa mazingira yalivyojitokeza. Kwa nini hili litokezee na Humoud aendelee kuvaa kinga ya Kibalozi, lakini pamoja na hayo baadae kutakuja suala.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wa Bara wametusaidiaje katika hili? Hilo ni suala naomba nielekeze katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Zanzibar kidiplomasia na Kimataifa inayotambulika ni Jamhuri ya Muungano ndio inayotambulika. Zanzibar katika hili hatuwezi kusimama kama Zanzibar, Zanzibar katika hili tutasimama kama Jamhuri ya Muungano.

Sasa suala naomba nijibiwe wenzetu Bara katika hili wametupa mchango gani, wametusaidiaje kwa sababu kuibiwa kwa nyaraka muhimu za Zanzibar katika diplomasia moja katika moja kati ya *Embassy* zilizopo hapa tungelihitaji kwa vyovyote vile kujua Tanzania imechukua hatua gani katika hili. Kwa sababu mimi naamini ingelikuwa hili lingelitokea Bara, tunakumbuka kwamba miaka ya karibuni fuvu la

Mkwawa lilikwenda likachukuliwa Ujerumani, likarejeshwa Tanzania. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja ama mawaziri baadae wanijibu hili.

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba Zanzibar tuna matatizo ya msingi na tutapaswa baadae tuweze kufikiria kinachotusibu Zanzibar ni nini? Ndani sisi wenyewe kwa wenyewe tunaibiana, wageni wanapokuja na wao ndio hivyo hutuibia, kwa lugha rahisi unaweza ukasema Zanzibar ni kama shamba la bibi anayetaka kwa kweli afanye chochote anachotaka.

Mhe. Naibu Spika, tokeo hili ukilitizama hasa ni aibu, ni tokeo la aibu, mgeni afike katika nchi hapa aende katika sehemu muhimu ya Makumbusho ya Taifa muhimu aibe nyaraka si siku moja, si siku mbili, si mwezi mmoja, si mwaka mmoja, tuna vyombo vya kiusalama katika kila taasisi, Usalama wa Taifa wapo katika kila taasisi, hivi watu hawa wanafanya kazi gani? Hawa Usalama wa Taifa tulionao hapa Zanzibar wanafanya kazi gani?

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi sishangai hata kidogo kwamba hata sisi wenyewe haya mambo hatuyapi umuhimu, mambo haya ya nyaraka, mambo haya ya magofu na mambo haya ya makumbusho hatuyapi umuhimu kama nchi, hatuyapi umuhimu tusidanganyane.

Sisi wenyewe humu Serikali wenyewe unaona lile Jumba la Makumbusho ni jumba la makaratasi mabovu hayana maana yoyote, hakuna anayejua umuhimu, hakuna anayejua thamani na laitani angelikuwa kuna mtu anayejua thamani leo Makumbusho ingelikuwa ni pahala nyeti miongoni mwa sehemu nyeti katika nchi hii. Lakini leo kila anayekuja tukiambiwa Makumbusho iko wapi, tukiambiwa Makumbusho ikoje katika hali gani, tutaona kwamba ni sawa sawa na idara yoyote ile iliyokuwa haina umuhimu wowote linatelekezwa tu. Kwa hiyo, matokeo haya yaliyotokea ni matokeo ya Serikali kutokuona umuhimu wa makumbusho na nyaraka za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema *security* tuliyonayo kwa kweli iko *weak* na ni *security* iliyokuwa haiangalii hasa masuala muhimu yenye moyo wa nchi, haiangalii. Tunachokiangalia pengine nani kazungumza na nani, nani anasema nini, nani anamsengenya nani, hiyo ndio *security* tuliyonayo. Lakini yale mambo ya msingi kabisa hayashughulikiwi, yaani mambo yenye uhai wa nchi na uhai wa Taifa hayashughulikiwi.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wameeleza lakini na nataka nieleze kwamba nyaraka hizi sisi wenyewe hatujui umuhimu wake, lakini nyaraka ndio nchi. Nchi zote duniani zingelikuwa hazipo kama zingelikuwa hazina nyaraka, nenda nchi yoyote, kinachoainisha kwamba hii ni nchi, hili ni Taifa ni nyaraka, nyaraka ndio zinazoonesha.

Kwa hiyo, utawala wowote, nchi yoyote kinacho-*determine* pale ni historia yake na nyaraka zilizopo. Maneno yametolewa hapa mgogoro wa Tanzania na Malawi, watu wanachokikimbilia ni kitu gani, watu wanachokikimbilia ni nyaraka, wameshafikishana mpaka wapi huko. Nyaraka ndio zinazozungumza kwamba mpaka unaishia wapi ingelikuwa hakuna nyaraka zinazoonesha hapo, nani angelisema na nani angelikuwa na hoja.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nyaraka hizi ukiachia mbali umuhimu wa nchi na historia yake, lakini vile vile nyaraka hizi ni muhimu kwa uchumi. Uchumi sasa hivi nyaraka ni uchumi, hawa walioiba msifikirie wanaiba nyaraka kwa ajili ya kwenda kufungia visheti, wameiba nyaraka kwa kuwa ni sehemu ya uchumi, ma-*researchers,* yaani watu wenye kufanya tafiti wanafanya kutokana na jamii tunayoishi.

Mhe. Naibu Spika, leo hatukuwepo miaka 1800 na hatukuwepo miaka 1700 anayeyajua hayo ni nyaraka ndio zinazoonesha hivyo. Tunayoyajua yalipita nyuma Mheshimiwa ni nyaraka kama leo kungelikuwa hakuna nyaraka leo tungelikuwa ni dunia gani. Kwa hivyo, nyaraka zina umuhimu na watafiti wote

wasomi wote wanafanya *PhDs* zao na kila kitu kutokana nyaraka. Ingelikuwa laitani tunafahamu umuhimu wa nyaraka watu wangelitoka Marekani wakaja hapa. Ukitaka kuijua Zanzibar, ukitaka kuijua Afrika Mashariki, ukitaka kujua eneo la Kusini mwa Afrika na utawala uliokuwepo zamani pahala pekee ambapo unaweza kupata maelezo hayo ni Zanzibar hakuna sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, msiwafanye watu wajinga wanaotoka kwa kutoka kwa ajili ya kuja kuiba nyaraka zile, zile ni mali kulikoni kitu chochote, ule utajiri kulikoni kitu chochote. Leo sisi wenyewe tunaona ni makarasi yanakaa ovyo ovyo tu weka Kilimani, weka Bwejuu  na weka wapi hatujui, watu wanasema "asiyejua maana wala usimwambie maana".

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, nasema nyaraka ni uchumi na ndio maana watu wakatoka walikotoka kwa ajili ya kuja kuchukua nyaraka. Lakini vile vile nyaraka ndio utawala wetu na sisi wengine tunaosema tunahitaji mamlaka kamili ya nchi hii ni kwa sababu hiyo kwamba tunafahamu kwamba Zanzibar ilikuwa ni nchi kulikoni nchi nyengine yoyote kwa Afrika ya Mashariki. Tunafahamu historia yetu, tunafahamu wapi tulikotoka, ndio maana sisi wengine mkatuona katika hili tumepagawa, hatuoni na hatusikii chochote, tunahitaji mamlaka kamili ya nchi yetu kwa mujibu wa nyaraka na historia tuliyonayo.

Tunaipuuza Zanzibar kwa kuiona tu ni kijinchi kipo kipo anayekitaka tu aje, haiwezekani. Zanzibar ni nchi kulikoni nchi nyengine yoyote Afrika ya Mashariki na *Inshaalah* kwa kumbukumbu hizi zinazoonekana ambazo tayari zimeshaibiwa baadhi ya watu wameshaanza kuziuza hizi, madalali wameshaanza kuziuza hizi, tunahitaji nyaraka hizi popote zilipo zirejeshwe hatuna *compromise* katika hili. Hii ndio historia yetu na hii ndio nchi yetu na haya ndio malalo yetu, hatuna pahali pa kitu changine kukieleza.

Mhe. Naibu Spika, bado narudia kwamba tulifika tulipofika kwa sababu moja tu, tulidharau magofu yetu ya kihistoria leo yapo wapi, Serikali imechukua juhudi gani katika hilio, Makumbusho yetu yako wapi na nyaraka zetu nazo hizo zimekwenda.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nasema katika hili tutasema mengi na katika hili tutawahusisha wengi, mimi sisemi nani ajiuzulu, sisemi kabisa. Lakini nasema ingelikuwa ni nchi ya kidemokrasia kikweli kweli, kwanza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais angelipasa kwa kweli ajiuzulu moja kwa moja.

Kwa sababu moja tu Mheshimiwa hili limetokea na hili kumbe vile Serikali inafahamu nini kilichokuwa kinaendelea na yeye ndiye aliyekuwa anaunganisha haya mambo ya Muungano na kuratibu shughuli za Muungano na mambo haya ya kidiplomasia ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hebu twambieni mmechukua hatua gani Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika hili, maana sisi hatutaki hadithi. Sisi tunahitaji hatua mulivyofanya na kilichoibiwa kisiendelee kuibiwa, lakini mpaka leo ni hadithi tu zinazokuja hapa. Leo yanabakishwa yale makaratasi tu yaliyokuwa hayana maana yoyote pengine, lakini zile karatasi muhimu nyeti zote zimeshakwenda.

Mhe. Naibu Spika, na Waziri aliyehusika na suala hili katika wizara inayohusika nae pia. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kazungumza pale tusioneee "madagaa tu", maana yake mimi hapa nahofia kwamba tukaja tukafika mahala kina Mwanakombo, Mwanajuma, akina Bahamadi, akina nani, watu wachache, lakini wale wenye dhamana watu waliohusika hawa ni muhimu vile vile kuwajibika. Tena wao waanze kwanza ndio baadae mdogo afuate, haiwezekani mkenda mkamuonea tarishi wakati huyu mwenye dhamana ambaye kapewa dhamana asimamie wizara ikawa yeye yupo tu haiwezekani.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi sisemi kwamba nani ajiuzulu wala, kwa sababu suala la kujiuzulu kwetu sie hamna. Mimi nasema tu ingelikuwa tuko katika nchi ya kidemokrasia kweli kweli, juzi mliona Marekani kule, kauliwa mtu mweusi lakini aliyeanza kuwajibika na Kamishna wa Polisi wa Jimbo zima la Marekani. Hivyo ndivyo watu wanavyokwenda, wala hana shindikizo wala chochote, hivyo ndivyo

nchi zinavyokwenda. Mimi nasema tu tusionee hawa watu wadogo wadogo wakati wakubwa kwanza wapo ambao walizembea dhamana zao mpaka wakasababisha Taifa liibiwe mambo muhimu katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuuliza suala katika *appendix* hizi za 56, Mhe. Waziri Haroun Ali Suleiman, alisema katika Baraza hili, kwamba nashukuru sana kwa michango kuhusiana na Jengo la Nyaraka au taasisi za nyaraka, mambo yaliyotokea pale ya wizi ni kweli Mhe. Waziri anatambiwa mambo yaliyotokea ni ya kweli yametokea wala hatuwezi kuyaficha na yamejadiliwa kwenye vikao vikubwa sana serikalini na Serikali ikaunda tume ikapeleka kule na tayari taarifa zote zimeshapatikana na wahusika wamekiri kwamba wamefanya makosa yale.

Sasa nataka nijue hawa wahusika waliokiri ni akina nani, naomba majina yao au kama ni hawa watatu tu tuambiwa au laa kama kuna na wengine pia tuambiwe. Kwa sababu taarifa nilizonazo wako wengine ambao wamekiri licha ya hao watatu, wako na wengine, sasa mbona waliotajwa humu ni watatu ambao ni wale madagaa tunaosema ni madagaa madogo.

Mhe. Naibu Spika, jengine inavyoonekana idara hii inakwenda na Maalim Haroun, Maalim Haroun anapokuwepo huku na idara hii inakuwepo huku, anapokwenda huku na inakuwepo huku, hii mahusiano yake ni yepi ya ku-*shift* idara hii kila Maalim Haroun anapokwenda, mahusiano yake ni yepi.

Lakini la mwisho, Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri tena na naomba niseme kwamba wote waliohusika hasa wale wenye dhamana watangulie wao kuwajibika kulikoni wengine na nasisitiza katika hili nyaraka zote hatuna *compromise* katika hili, hayo ni mambo ya kidiplomasia, Serikali ina uwezo kamili kufanya utafiti wakajua nyaraka ziko wapi na popote pale zilipo, tunahitaji nyaraka zetu zirejeshwe nchini na Serikali ije ituletee hizo.

Mwisho kabisa naunga mkono hoja ya kamati, kamati nawashukuruni sana kwa kazi nzuri mliofanya. Ahsanteni *(Makofi)*

**Mhe. Abdalla Mohammed Ali:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipatia fursa ya kusema machache katika ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyekiti kwa kazi yake iliyochukua wiki sita na ugumu mkubwa wa kazi hii. Lakini pia namshukuru vile vile kwamba alifika pahali akaona kazi yangu nahitaji wataalam, kwa hivyo, na wataalam aliowaomba walitoka hapa hapa Baraza la Wawakilishi na aliona nitamfaa katika kuendeleza kazi hiyo. Kwa hivyo, akaniajiri rasmi kwamba ni mtaalam katika kumsaidia kufanya kazi yake, kwanza namshukuru kwa hilo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini wiki iliyopita na leo Jumamosi tunaendeleza kupitia Ripoti za Kamati na hii ni moja kati ya Ripoti za Kamati. Majibu tunayoyapata tumeshaona na tunayasikia na ninachotaka kusema ni kwamba tunaona jinsi gani Serikali inavyowajibika, kama tunaridhika nayo majibu ya Serikali sawa, kama haturidhiki nayo...Wazungu wanasema ni *upto us,* yaani ni wajibu wetu sisi sasa kuamua kwamba tunawajibika au tunaridhika au haturidhiki na Kanuni zipo zinazoweza kutumika kwa kufanya kazi yetu sawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, nimewasikia wajumbe wengi wakizungumzia hapa na wengi tumejenga dhana kwamba kuna bwana anayeitwa Humoud, yeye anahusika labda na upotevu. Mimi sisemi wizi kwa asababu sio Mahakama, nasema upotevu wa nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, katika ripoti iliyokabidhiwa hapa ina vielelezo, na moja kati ya vielelezo hivi ni KTN nambari 25. Kielelezo hiki kinahusu barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Utamaduni na Michezo inayotoka Ubalozi wa Oman.

Mhe. Naibu Spika, barua hii anaombewa na Ubalozi wa Oman mfanyakazi mmoja ambaye anakuja kufanya kazi naomba niisome.

"Ubalozi mdogo wa Oman hapa Zanzibar una furaha kukusalimia na kukujuilisha kuwa Wizara ya Mila na Utamaduni nchini Oman inatarajia kumleta hapa Zanzibar, Bwana Humud Abdalla Rashid tarehe 15 mwezi wa Julai kuja kuendeleza kazi za udhibiti na uhifadhi wa nyaraka zinazohusu historia ya Oman. Pia Wizara hiyo ya Utamaduni ya Oman inatoa baadhi ya vifaa vya kuendeleza uhifadhi huo kama zawadi kupitia kwa Bwana Humud".

Sasa nijiulize kwanza hivi vifaa kwa barua hii vinatoka Ubalozi wa Oman au vilikuwa vinatoka kwa mwenyewe Humud, lakini barua hii ilitaka kuendeleza kazi fulani, labda niulize ubalozi huu wa Oman umeshaleta barua nyengine ya kumsitisha kazi au kuomba kwamba wao kazi yao imeshamaliza hapa Zanzibar, kwa maana Bwana Humud ameshaondoka rasmi na haendelei tena na kazi hii?

Jengine ni kwamba pia *memorandum of understanding* ambayo Serikali ya Oman ilitiliana saini na Wizara ya Elimu Zanzibar, kwamba wao katika majukumu watakayoyafanya kazi zao ni *exchange of photocopies of documents and manuscripts relating to Zanzibar and Oman in both countries*. Hii ndio *memorandum of understanding* ilivyosema.

Sasa labda niulize katika kipindi chote ambacho Bwana Humud alikuwa ameruhusika kufanya hii kazi, kazi ya *exchange of information* au *exchange of photocopies* pia nayo iliendelea kwa kipindi hicho? Au yeye baada ya kufikisha hivyo vifaa hii kazi haikufanywa.

Lakini kuna mengi humu yaliyopendekezwa mengine ni *exchange of information and publication between the National Libraries of the two countries,* sisi tulipata chochote? Kwa sababu na sisi ilikuwa tupate kutoka Oman mbali na hizo *camera* za *CCTV*, tulipata vyengine kutoka huo ubalozi wa Oman?

Jengine *hold cultural and arts with exhibition into the two countries*, hiki pia kilipatikana? Yaani watu wetu hapa walitoka wakaenda kule na wao wakaja huku kwa makubaliano haya yaliofikiwa.

Sasa lakini hoja kuu je, sisi tumeshapata barua rasmi ya kufikisha kazi ya Bwana Humud kwamba yeye haendelei tena na kazi hii ya kuhifadhi nyaraka zetu hapa Zanzibar, kazi hii imemalizika? Je, ubalozi kama imemalizika umeshatupa barua rasmi kwamba yeye ameshamaliza kazi na kaondoka au kaondoka kinyemela tu?

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nachangia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala nilisema hapa kwamba, mimi naona ule umuhimu serikali haijauweka wa nyaraka kujua kwamba labda zina umuhimu gani.

Mhe. Waziri wakati alipokuwa anakuja kujibu hoja alisema kwamba serikali inauona umuhimu huo, lakini nashukuru kwamba kamati wao wenyewe au kamati imekuja kuonesha kwamba serikali haikuweka umuhimu katika mambo ya nyaraka na matokeo yake ni kama haya yaliyotokea.

Mhe. Naibu Spika, wengine wamesema hapa kwamba pasije pakakamatwa vidagaa mapapa wakaachwa. Mimi naomba nitoe mfano mdogo tu wa mwandishi mmoja wa kitabu cha Kiingereza. Mwandishi huyu yeye anaitwa George Orwell, aliandika kitabu kikaitwa *"Animal Farm"* ambacho kwa miaka ya nyuma Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano Mwalimu Nyerere alikipiga marufuku.

Mwandishi huyu alisema kwamba, aliwaweka kama wanyama katika kundi moja na wanyama wakawa wana mawazo kwamba wao wote ni sawa, *all animals* wakasema kwamba *all animals are equal*. Lakini katika maisha yao wakahisi kwamba kuna mnyama mmoja yeye anapata vitu vingi zaidi, kuanzia hapo

wakaanza kuibadilisha wakasema aa sasa tubadilishe, wakasema *all animals are equal, but some animals are more equal than others*, kwa sababu wengine wao watakuwa wako zaidi kuliko wengine. Hapo ndio mchafuko ulipoanza.

Sasa na hii nasema tu kwamba yeye alichukua mifano hii ili tuitumie katika maisha yetu, kwamba kama sheria ipo basi sheria iwe sawa kwa wote isije ikabagua. Hivyo ndivyo alivyotuusia mwandishi wa kitabu, na nakumbusha tu kwamba kitabu hiki kilipigwa marufuku Tanganyika kisije kwa sababu ya maudhui yake.

Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu kidogo tu yale ambayo nilikuwa nayasema mwanzo kwamba, tunahitaji serikali iliyo makini.

Moja katika mapendekezo waliyosema hapa wao wamesema kutochukuliwa kwa hatua zinazostahiki kwa matokeo ya upotevu wa nyaraka kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, mikataba hii, *memorandum* hizi za *understanding* zipo na mkataba huu wa kuombewa Humud kuja kufanya kazi ni mwaka 2005, lakini leo ni mwaka 2015 miaka kumi. Sasa kama kumechopolewa chopolewa sijui kwa muda wote huu kumechopolewa kiasi gani.

Katika kipengele hiki kutochukuliwa hatua ripoti ndio inasema;

"Imebainika kwamba makosa kama hayo yamewahi kutokea mara kadhaa katika miaka ya nyuma na wahusika hawakuchukuliwa hatua zinazostahiki".

Ndio yale tunayoyasema Mhe. Naibu Spika, kwamba kutokuchukua hatua kwa kosa dogo ndiko kunakosababisha makosa makubwa yakatokea.

Leo tumeona kwamba kuna makosa huko nyuma mengi yametokea lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Waswahili wanasema ukimpa nini ile anahitaji nimeisahau, leo unampa mtu panga tu lile atataka nini. Sasa haya ndio yaliyotufikia kwamba tunachelewa kuchukua hatua kwa wale ambao tunahisi wamefanya uoza katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, pia hapa inasema kutokuwepo kwa mpango imara wa udhibiti wa usalama wa nyumba ya nyaraka na usimamizi na uendeshaji wa ofisi ya nyaraka.
Kamati imesema kwamba; "Hata hivyo, kamati imebaini kwamba kuna ukiukwaji mkubwa wa utaratibu wa usimamizi wa uendeshaji wa taasisi iliyowekwa na sheria hii, hasa kwa upande wa uongozi". Kuanzia 2005 mambo hayo yanajitokeza leo 2015 unakuja kulia nyaraka hazipo!

Mimi nilikuwepo katika kamati hii kwa muda mfupi, na kwa ujumla nilipata bahati ya kulinganisha. Kwa sababu nimepata bahati ya kutembelea *London Archives* nchini Uingereza, nilikwenda na katika masomo yangu nikabahatika kwenda kufanya *comparative* au *comparison*.

Sasa nilivyovikuta katika hii *National Archives* yetu ni *quite different*, naweza kusema kwamba tungepata muda Baraza likatupeleka kule tukafanya ulinganisho kati ya nyaraka zilizoko *London Archives* na nyaraka zilizopo *Zanzibar Archives,* Wajumbe naona wangezidi kusema hapa kama wangelia labda wangeamua kuondoka hasa katika Baraza lako, hamna kitu, kuna nyaraka muhimu hazipo. Sasa hiyo ndio inaonesha tu kwamba sisi ule umuhimu wa nyaraka hatuna.

Mhe. Naibu Spika, juzi Tunisia na nashukuru kwamba na mimi pia nilipata bahati ya kutembelea, *museum* moja lilipigwa bomu lakini kutokana na ule umuhimu wa *museum* hii basi baada ya wiki moja tayari kumeshajengwa jumba la kisasa ili zile zilizobakia zihifadhike pale, *museum* ya Tunisia. Lakini leo

unakwenda kukuta ukienda *Archives* kuna kontena huko nyuma unaambiwa sijui miaka mingapi halijafunguliwa.

Sasa ukija ukisema hapa waziri atakuja kusimama aseme anavyotaka yeye kwa sababu yeye ndiye msemaji wa mwisho.

Mhe. Naibu Spika, kama kweli tunataka kuweka hii *Archives* katika usalama basi tunahitaji hatua zilizopendekezwa humu na kamati hii zifikiwe, si hivyo itakuwa tunasema tu waraka huu uko wapi, umeshachanika hauna maana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri kwa hayo machache naunga mkono ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia asubuhi hii kuwa mimi na nyinyi hali ya afya na uzima na kuweza kuendeleza shughuli za Baraza katika siku ambayo si miongoni mwa kazi za Baraza.

Pia nikushukuru na wewe kuweza kunipatia nafasi hii na mimi nikaweza kutoa mawazo yangu machache katika ripoti hii ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, jana ilipokuwa ikisomwa ripoti hii wengi wetu tuliondoka hapa vichwa vinatuuma kutokana na kadhia iliyofanyika katika nyumba hii ya Nyaraka.

Nyaraka ndio rasilimali ya nchi yoyote ile duniani, nyaraka ndio kitambulisho cha nchi husika na mambo yaliyomo ndani ya nchi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi kila nikikaa hukumbuka mawazo ya Mwalimu Nyerere aliposema kwamba Wazanzibari uchumi tunao lakini tunaukalia. Hii ina tafsiri pana sana, sasa bado sisi Wazanzibari tunazifanya kama nyaraka ni karatasi tu hivi, zilizoandikwa zamani kama vile tunavyozifanya hadithi za kale, lakini nyaraka ni uchumi wa nchi.

Jana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule aliposoma hotuba yake hii kwa hapa Zanzibar alisema watu wawili tu ndio waliowahi kwenda kujifunza pale kwenye Nyaraka; mmoja ni aliyekuwa Waziri Kiongozi wakati huo wa mwanzoni, Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Rais wa Awamu ya Tano, Mhe. Salmin Amour Juma.

Hao waliwahi kupita pale na faida ya Waziri Kiongozi huyu ameelimisha jamii, historia ameitoa vya kutosha kwa Wazanzibari ili tujue na Zanzibar yao ilivyo, ilivyokuwa na inavyoendelea kuukosa ule uzanzibari wao. Kwa hivyo, kitu nyaraka ni kumbukumbu tosha, hivyo Mwenyezi Mungu ametuwekea vielelezo.

Mhe. Naibu Spika, nitakupeni mfano, Mwenyezi Mungu ameteremsha Qur-ani. Qur-ani iliteremshwa wakati wa Mtume Muhammad (*S.A.W*), Maswahaba wakaiandika ile Qur-ani mpaka ikakusanywa katika kitu kimoja unaitwa msahafu. Kama ulikuwa haupo msahafu waislamu na mataifa mengine na watu wengine tusingelijua jinsi Mwenyezi Mungu alivyouandaa huu ulimwengu. Lakini Msahafu umekusanya hayo tunajua toka dunia ilipoumbwa kwamba Mwenyezi Mungu amesema ameumba ulimwengu kwa muda wa siku sita, siku sita hizo akaingiza mambo yote, msahafu umetuelekeza hivyo. Kwa hivyo, hizo ni kumbukumbu za kufahamu.

Msahafu huo umeeleza kwamba Mwenyezi Mungu ameumba moto na pepo, ni kumbukumbu za enzi hizo, lakini Waislamu kwa kuhifadhi Msahafu huu mpaka leo kizazi kilichopo na kijacho wanajua kwamba Mwenyezi Mungu ameelekeza nini.

Kwa hivyo, hizi ni jumla ya kumbukumbu, na nchi wameiga kutoka kwa Mwenyezi Mungu na wao wakasema kila linalofanyika tuandike na tuweke kumbukumbu. *Alhamdulillah* Zanzibar imesifiwa kwamba ni nchi za mwanzo kabisa duniani zilizoanza kuweka kumbukumbu zake.

Mhe. Naibu Spika, lakini katika kuangalia kwangu humu nimeona kwamba kuna kumbukumbu zimeibiwa kuanzia mwaka 1219, huu ni muda mrefu sana hizi zote zimeibiwa 1240 zimeibiwa mpaka tukafika katika kumbukumbu nyengine za mwaka 1897.

Jumla ya kumbukumbu hizo zote za enzi na enzi tayari hazionekani nchini, huku ni kuua nchi ya Zanzibar, ni kuua historia ya Zanzibar, ni kuua kila kile ambacho Zanzibar kilijifanyia na kuweka kumbukumbu zake na hatima yake kwa uzembe huu tunaouendeleza kuona kama ah, hizi ni karatasi tu.

Jamani hapa tunapoishi kwa kutojali haya kama Zanzibar sasa hivi tumeacha mambo ya msingi tumeweka siasa mbele, badala ya kushughulikia mambo ya msingi tumeweka siasa mbele kuliko nchi, tutafika wapi?

Mhe. Naibu Spika, tutafika wapi kwamba mambo yote ya muhimu hatuna habari nayo, ni siasa tu. Watu wanakuja na ujanja ujanja tunakubali kirahisi, mtu akishaambiwa hapo utapata asilimia yako kumi sisi basi tunatosheka na asilimia kumi, tunauza yale ambayo ni muongozo wa nchi yetu hii. Hatufiki, hili ni tatizo sugu, kwa sababu Zanzibar hivi sasa tunajua kwamba Mwenyezi Mungu alipoiumba njaa, aliiumba njaa maskani yake ni tumboni, ndio maskani ya njaa inapoishi. Lakini sisi watu wa leo tunayahamisha yale maskani ya njaa tumeyatoa katika tumbo tumeyaweka kichwani. Sasa njaa ukiiondosha tumboni ya kuiweka kichwani huna lolote utakalolifanya isipokuwa sasa wazo lako ni wizi na mambo mengine, utauza mpaka kisichouzika, na hii ndio hatua tuliyofikia. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jana hapa Mhe. Mwenyekiti, sijui sijaifahamu vizuri lakini alisema kumbukumbu za kijerumani zote hazipo tena hapa Zanzibar ziko Ujerumani, zote ni historia kwa Zanzibar lakini hazipatikani. Sasa hivi ukitaka kusoma historia uondoke Zanzibar ukasome Ujerumani, *what is this!*

Sasa itabidi Mzanzibari akitaka historia ya Zanzibar aondoke Zanzibar aende Oman au Uingereza. Vitu ambavyo vilikuwa vimekaa kitako hapa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, huu ni uzembe, uzembe kabisa!
Kwa hivyo, nchi ndio muhimu kuliko siasa, nchi ndio muhimu kuliko jambo jengine lolote. Kutokana na hali hii tunayoendelea nayo Mhe. Naibu Spika, itafika siku tutaambiwa kuwa hapa Zanzibar si petu, itafika siku tuambiwe kuwa Zanzibar si yetu, na dalili hizo zinajionesha zinakuja hizo. Itafika siku ataanziwa Rais ataambiwa hapa Ikulu unapokaa si pako, hama, kwa uzembe huu huu unaondelea.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, waswahili walisema *"Mchelea mwana kulia yeye"*. Kwa hivyo, tujengeni huruma tu, watu wanafanya madhambi tuwafutie madhambi yao tu, hatima yake tutakuja kulia sisi. Kwa hivyo, naiomba sana serikali, hili si suala la kulifumbia macho, ni lazima tuoneshe umahiri na umadhubuti wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni kabisa tumesikia vyombo vya Habari, Wakenya wanadai kwamba Pemba ni yao, juzi tu. Ukaanza mgogoro ukaanza kuvutwa vutwa hapa lakini tunashukuru *alhamdulillah* katika kamati ilipofanya kazi kumbukumbu hizi wamezigundua kwamba hiyo Mombasa ni mali ya Zanzibar, kwa hivyo bado hizi kumbukumbu hizi zipo, na tushukuru kwamba kuna Fungu Mbaraka bado kumbukumbu hizi Waheshimiwa wamezikuta bado zipo, hayo ni madai. Lakini kwa kumuacha mwana akawa analia tukawa tunambembeleza hatima yake kila kitu hapa kitaondoka.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana viongozi; uzalendo wa nchi ni lazima tuupe kipaumbele, kama hatukuupa kipaumbele nchi yetu tukang'ang'ania siasa tu, siasa ni kitu chenye kuondoka, lakini kizazi chetu kinachokuja mimi naamini sisi sote tuliomo katika Baraza hili, sote hatutoshuhudia elfu mia tatu (3000) hatutoishuhudia sote hapa. Na hichi kizazi chetu tulichokizaa kilichopo watu walio na mwaka mmoja hadi kuendelea hawatoushuhudia mwaka wa elfu tatu (3000), kwa sababu miaka thamanini na tano (85) ni umri mkubwa kwa uhai wa leo.

Sasa angalia kizazi kitakachokuja hicho kumbukumbu hizi hazipo na nyengine ndio zinazidi kuchukuliwa watakujafanya nini katika nchi yao, hili ni suala la kujiuliza sote.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi niitake serikali hasa wizara inayohusika na mambo haya ifanye wajibu wake.
Mhe. Naibu Spika, mimi siamini kwamba hawa waliotajwa kwenye kamati; Mwanakombo sijui na nani kwamba ndio hao. Mimi hilo siamini, na haiwezekani bwana mtaka nyaraka atoe kauli kuwajibu hawa kwamba mutaboreka kama wanavyoboreka mabosi wenu halafu kwamba mabosi wameboreka sisi tukasema kwamba hizi ni kauli ambazo hazina uhakika, mimi hili pia siamini.

Ni vyema kauli hii ya bwana Humoud kuangaliwa, hawa mabosi wakoje, wafuatiliwe bosi mmoja mmoja kuonekana ile hali yao wakoje.

Inawezekana kwamba hawa maisha yao mazuri tu, inawezekana pengine lakini pia inakuwa haiwezekani. Pale utakapofanywa uchunguzi wakaona kwamba hali zao za maisha kwamba ni duni itakuwa wahusika kweli ni hawa, lakini tukisema kwamba hatufuati haya maneno wala hatuwafanyii uchunguzi hawa mabosi, basi itakuwa hawa wawili tumewaonea.

Kwa hali yoyote Mhe. Naibu Spika, maelezo yaliomo humu kwamba watu wanaonekana wanaingia na mikoba wakitoka na mikoba imenona bila ya kufuatiliwa chochote. Mimi niulize hii kazi ya ulinzi na usalama wa nchi hii kazi yake ni nini? Au siasa tu, yule kapigiwa jungu hili yule kafanyiwa hivi, Waheshimiwa chonde chonde, nchi inakwenda haya, tuendeleeni na siasa!

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi naunga mkono *mia fil mia* ndani ya Ripoti ya Kamati Teule. Ahsante sana.(*Makofi*).

**Mhe. Subeit Khamis Faki:**Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia ripoti hii ya Kamati Teule ya Upotevu wa Nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwapongeze Kamati hii Teule ambayo kuwa Mwenyekiti wake ni Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, kwa kweli niwapongeze na niwasifu kama wamefanya kazi nzuri, wametimiza wajibu wao wametueleza cha kutueleza, aliyekuwa hakifahamu sasa amefahamu kama kuna nini.

Mhe. Naibu Spika, masikitiko yangu mimi kwanza naomba sana masikitiko yangu nielekeze kwa serikali yetu. Upotevu huu wa nyaraka kwa sababu nyaraka ni vitu muhimu sana, na umuhimu wa nyaraka umeonekana kwa yule mtu mfano akiwa na kitu chake ukapotea waraka wake anaweza akafilisiwa au akanyang'anywa hivi hivi kitu chake anakiona, na ndio maana kutokana na hizi nyaraka imekuja sasa hivi hata mtu binafsi akizaliwa inabidi awe na cheti cha kuzaliwa, kwa sababu kile sawa sawa na waraka wake wa kuonesha uzawa wake na makuaji yake na miaka yake katika uhai wake.

Sasa Mhe. Naibu Spika, vitu kama nyaraka za serikali, leo nyaraka za serikali zinapotea hivi hivi kwa kuibiwa. Mimi nasikitika sana, tena nasikitika sana. Nasikitika na serikali yetu kama kweli serikali sijui

niseme imelala au niseme vipi. Na mimi naomba niseme kama wanavyosema wenzangu siasa tukiiendekeza mno basi itatupeleka sipo.
Leo nyaraka muhimu za serikali zinapotea kwa kuibiwa, hivi serikali walikuwa wako wapi mpaka nyaraka hizi ziibiwe tena nyingi sio kidogo, tena nyaraka hizi zimeibiwa na mtu ambaye anakuja mara kwa mara Zanzibar, anachukua kidogo anaondoka, ananyofua anakwenda zake, anakuja kuchukua tena, serikali haipo, kama hatuna vyombo vya ulinzi, hapa naona kuna hii ripoti ya Polisi ya kuthibitisha, leo wametajwa hawa akina Mwanakombo na mwengine nimeona hii ripoti ya Polisi ambayo kuwa wameiona wenzetu hawa wa Kamati.

Leo nyaraka muhimu za serikali hazipo, zimeibiwa na mtu, tena nyaraka ambazo zinathibitisha uhai wa nchi yetu.
Mhe. Naibu Spika, mimi naona hapa pana usiri mkubwa, serikali bado haijataka kutwambia, hebu itwambie ukweli kuna nini? Mimi naomba tuambiwe kuna nini?

Leo nyaraka kama hizi muhimu mpaka zinakwenda hazipo sasa hivi tunaanza kutafuta njia. Naomba sana serikali, kwa hili basi ifanye jitihada kubwa kama hapa pana usiri fulani basi ubainike kama kuna usiri gani. Kwa sababu haiwezekani nyaraka za nchi zipotee hivi hivi duuu! Waheshimiwa si jambo la mas-hara hili, si masihara, wenzangu wamesema na mimi nasema wanaweza wakaja watu wakatwambia hapa si kwenu, kwa sababu nyaraka mtu kaziiba na akishaziiba anaweza akazitengeneza vizuri akija atakwambia mimi ndiey mwenyewe na waraka huu ninao utasema nini wewe? Keshazitengeneza mwenyewe anavyojua, anakuja na waraka anakwambia nchi hii si yako mimi waraka wangu huu, wewe utasema nini na huna waraka wewe, mkienda mahakamani hata huko Umoja wa Mataifa inayotizamwa ni waraka, yeye anathibitisha kwamba waraka wangu huu wenu nyinyi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wa kuthibitisha kwamba hii nchi kuwa ni yenu uko wapi?

Leo nyaraka hazipo, tumekaa tu hivi hivi tunatafuta huyu Humoud mwenyewe alikuja akichukua ananyofoa anaondoka, leo tunatafuta kwa sababu anafanya kazi ubalozi, tunatafuta njia sasa.

Tutafute njia gani ya kumdhibiti Humoud, Waheshimiwa inasikitisha sana haki ya Mungu inasikitisha! Vitu muhimu kama nyaraka za nchi anakuja mtu hawa watendaji waliokuwa wakipewa pesa wanagaiwa pesa kama pipi wananyofoa karatasi muhimu wanatoa, jamani tunaelekea wapi wenzangu? Hii nchi tunaipeleka wapi? Anakuja mtu anagaiwa pesa tena mtu wenyewe anapewa shilingi elfu ishirini, kuna mmoja humu kwenye ripoti anasema alikwenda akawekwa halipogaiwa alipewa elfu ishirini, elfu ishirini unatoa waraka wa nchi?

Juzi kama alivyosema mwenzangu ulikuja mgogoro wa Kenya wakasema kwamba Pemba ni ya kwao, ingekuwa hatuna vidhibiti wale Kenya wanao waraka wanaothibitisha kama Pemba ni yao ingekuwa ni yao kweli. Lakini kwa sababu tunao waraka siku ngapi ndugu zetu hapa wa Tanzania Bara jirani zetu saa hizi tunawaniana ile Fungu ya Ndege, ndio Fungu Mbaraka watu wanasema Fungu ya Ndege ndio ufupi wake, si kisiwa cha ndege kile, sasa tunawaniana hivi sasa.

Hivi sasa inasemekana wenzetu wanakwenda kunyofoa nyofoa wanatafuta mafuta kule ili wakifanye kama chao. Lakini kwa sababu tuna udhibiti wakati wowote hatujataka ni sisi wenyewe ulaini wetu, lakini kama si ulaini wetu tukijitutumua kidogo tu kule wataondoka na magari yao, hayo mameli yao wanakwenda kutafuta. Lakini kwa sababu tuna vidhibiti, leo vidhibiti vya nchi vinapotea kwa watu wanakuja, watu wananyofolewa pesa mbili mbili serikali itwambie imechukua hatua gani kutokana na suala hili, kwa sababu hili suala si la leo.

Lakini kama ni ushahidi wa Polisi, je, kuna utaratibu gani tena unaochukuliwa na serikali kuona kama nyaraka hizi kuna umuhimu wa kupatikana. Kwa sababu tuelezwe, sio kwa sababu zimeshachukuliwa

ndio tukae tu hivi tutakuja kuuzwa na nchi yetu hii, kama tushauzwa ndio hivyo tumeshauzwa na nchi yetu tutamaliza kuuzwa na nchi yetu.
Sasa kabla ya kumalizika kuuzwa, serikali itwambie imechukua jitihada gani na itachukua jitihada gani na itafanya jitihada gani kuona kama nyaraka hizi zinarudi Zanzibar, sio kama zimeshapotea tena ikawa nguvu za "*mtokomele*" humu sio nguvu za "*mtokomele*" hizo.
Waheshimiwa naomba sana serikali, naiomba sana wanaowajibika wale viongozi wa juu wawajibike kuona kwamba suala tena serikali ifanye kazi kweli kweli si suala la masihara hili. Jamani mambo mengine tusifanyeni masihara, lazima serikali yetu iwe *serious* kutokana na vitu kama hivi muhimu nyaraka za serikali.

Kwanza naomba serikali sana, hilo jumba la Makumbusho ambayo ni sehemu zinazohifadhiwa nyaraka isiwekwe tu hivi hivi, iwe na ulinzi na inatakiwa iwe na vitu ambavyo wanavyoita wenzetu vya kisasa, mtu anaingia mule anaonekana anachokifanya, anaingia anatoka anaonekana anachokifanya.

Leo anaingia mtu na mkoba wa ukili anachukua nyaraka muhimu ushahidi wowote hatuna, duh! Jamani tusifanye kama hivi .(*Makofi*).

Serikali jamani msifanye masihara na mambo kama hayo muhimu, sisi tunakuja kupiga kelele humu kwa mambo muhimu sana. Tunaomba sana michango yetu tukichangia ya serikali ifanye kazi kuifanyia kazi, tusije tukisema humu halafu serikali ikawa haifanyii kazi.

Tunaomba sana vitu kama vile muhimu, tunaomba sana pawekwe vyombo vya kisasa, anayeingia awe anaonekana na anachokichukua anaonekana, na saa anayochukua anaonekana.

Hizi zimeshachukuliwa, lakini bado watu hawajatosheka, na hizo wanazochukua kwa sababu wana haja ya kuhodhi hii nchi wanaweza wakarudi tena, wajanja wakaja kuchukua tena.

Kwa hiyo, kile kilichopo kwanza tukihifadhi na hizi zilizochukuliwa serikali ifanye jitihada ya kuona kwamba uhakika nyaraka hizi zimerudi katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu sio mkubwa kwa leo, nilikuwa nataka na mimi nitoe dukuduku langu kutokana na suala hili, na kutokana na hayo machache ninayoyazungumza.

Mimi naunga mkono Ripoti ya Kamati baada ya mia naunga mia na hamsini. (*Makofi*).

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Naibu Spika, na mimi kabla sijaanza lolote, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na uhai na leo nipo katika kutekeleza majumu waliyonikabidhi wananchi wa jimbo la Kwahani.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nianze kwa kulipongeza Baraza lako Tukufu kwa kukubali baada ya hoja za Wajumbe akiwemo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ya kutaka kuundwa Kamati Teule, na Baraza lako likakubali kuundwa kamati ile.

Imani yangu kwamba Baraza lingesema hakuna haja basi haya yote ambayo leo tunazungumza hapa tusingeyajua wala tusingeyafahamu.

Sasa nitoe shukurani zangu za dhati kwako kwa Baraza lako kukubali chini ya uongozi wa Mhe. Spika, kuunda kamati ile Teule.

La pili Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kuipongeza Kamati Teule ambayo iliongozwa chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ambaye pia ni Mwenyekiti

wa Baraza na Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa namna ambavyo wamefanya kazi kubwa, na wamejitahidi kadiri ya uwezo wao kutuletea kitu ambacho leo hii tunakichangia kwa hamasa kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, jana alimaliza muda wake wote kwa kusoma hii, na sisi kama tutaanza kupitia kifungu baada ya kifungu sitegemei kama tutaweza kumaliza michango yote. Sasa imani yetu kwamba, na hata na mimi nitajaribu kuchangia kwa ujumla tu yale ambayo nahisi naweza kuyachangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi baada ya kukipitia kitabu hiki nilijaribu kuangalia kasoro za kiutendaji ya kiofisi, na baadhi ya kasoro ambazo zimeandika katika aina mbali mbali, na tumepata kuona udhaifu wa wafanyakazi wetu katika namna ambayo kwa utendaji wao wanavyofanya.
Mhe. Naibu Spika, mimi nakuwa napata tabu sana, tunaunda Kamati Teule inafanya kazi, inapoteza muda, inapoteza nguvu kwa muda mrefu, *then* tunakuwa tunatumia kodi ya wananchi katika kufanya kazi zao katika kipindi chote.

Sasa wanapotuletea taarifa mimi sitaki kuwarekebisha wenzangu, lakini ningeomba zaidi tuziangalie taratibu za kisheria, kuona namna gani tunaweza kuisaidia hii taarifa ya Kamati Teule katika kupendekeza kwa Serikali kuchukua hatua kwa wale waliohusika. Kwani hilo ndilo ambalo linaweza kutusaidia na kuweka sawa yale madhaifu ambayo yamejitokeza.

Mhe. Naibu Spika, hata mimi nadhani kabisa kitendo cha kuibiwa nyaraka za Serikali, kwa sababu kinaweza kutupelekea na kutuweka katika mazingira mabaya. Tunapoteza kumbukumbu za nchi, wanapoteza historia lakini tunapoteza mambo muhimu ambayo yanaweza siku za mbele kushindwa kuyapatia ufumbuzi kutokana na kupata uthibitisho wa nyaraka, lakini na wakati huo huo haupo.

Sasa na mimi kwa hili la wizi wa nyaraka, ninaungana na wale wote ambao waliokuwa wanapiga vita suala la wizi wa nyaraka, wanapiga vita suala la wafanyakazi wasio waadilifu.

Mhe. Naibu Spika, chengine nilikuwa ninajiuliza mimi nilikuwa ninataka nimnukuu huyu Humoud, na nilikuwa ninajaribu kupitia *data* mbali mbali au taarifa mbali mbali, nimepitia taarifa za Mhe. Waziri, nimepitia taarifa za Kamishna wa Polisi nimeona hapa.

Sasa huwa ninapata tabu juu ya suala la Humoud, lakini kama nilivyosema kwamba taarifa tumepata, na nina imani kwamba Wajumbe wenzangu namna walivyochangia basi nchi hii inaongozwa kwa taratibu za sheria, na nina imani kwamba Serikali hii itafuata sheria kuona hatua za sheria zinachukuliwa kwa kila aliyehusika.

Mhe. Naibu Spika, ukiachilia Ndugu Humoud namna alivyozungumziwa na tumekuwa tunapata tabu, wengine mpaka tunafika pahala tunavuka mipaka ya kuzungumza. Unajiuliza, maana yake kwa sababu sisi tunapata hofu katika suala la Humoud kwamba Humoud aliiba kama Humoud au ametumwa. Sasa hii ndiyo pale tunaposema kwamba tuna imani kwamba Serikali itakapoanza kuchukua hatua za kisheria na kumpata Humoud na kumdadasi, na kama maelekezo ya Waheshimiwa Wajumbe walivyosema, lazima huyu mtu akamatwe na baada ya kukamatwa hatua za kisheria zichukuliwe.

Mhe. Naibu Spika, hofu yangu tusije tukafikia pahala tukaacha kumzungumzia Humoud, tukawa tunaizungumzia Oman na hii ni hatari. Kwa sababu hatujajua hasa Humoud amelifanya tendo hili kwa dhamira gani. Sasa ni imani yangu, kwamba taratibu za kisheria zitakapofanyika basi ukweli utadhihirika. Kwa sababu tunaanza kuizungumzia Oman, inaweza ikatufikisha pahala tukaharibu mahusiano na ndugu zetu wa muda mrefu kwa sababu ya mtu mmoja kwa dhamira yake yeye mwenyewe.

Sasa niiombe sana Serikali, baada ya ripoti hii kupokewa na Wajumbe kulifanyia kazi suala hili kwa haraka. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Naibu Spika, sababu ya kusema hivi kwamba hofu ya kumuacha Humoud na kuanza kuizungumzia Oman, kwa sababu hata mijadala yetu nayo inaonekana inakwenda katika mwelekeo huo huo.

Badala ya kuizungumzia ripoti, tunaanza kuzungumza masuala ya kisiasa kwamba ooh! hapa mchezo huu unaonekana ni wa kisiasa, watu wameweka ndugu zao. Sasa ninasema katika masuala ya kisheria hayana ndugu, hayana mjomba. Sasa hofu hii ndiyo iliyonipelekea Mhe. Naibu Spika, ya kuzungumzia suala hilo, kwamba tukiacha kuzungumzia Humoud, tunazungumza kuhusu Oman. *(Makofi).*

Sasa ninafikiri Wajumbe na sisi baada ya kuacha kuzungumzia ripoti na kuitaka Serikali iyafanyie kazi yale ambayo Kamati Teule imeyapendekeza, tunaanza kuzungumzia masuala ya kisiasa, na wengine wakafika pahala hata kuwataka viongozi wakuu wajiuzulu. Lakini hiyo sisi kama wanasiasa tumeshaizoea, kwa sababu hiyo ndiyo nyimbo ya wenzetu kwenye masuala ya kuwa Makamu wa Rais ajiuzulu, kwenye kuchangia Miswada Makamu wa Rais ajiuzulu, kwenye kuchangia ripoti za Kamati Teule ajiuzulu.

Sasa ni nyimbo ya wanasiasa tumeshaizoea. Hakuna jambo hata moja Mhe. Naibu Spika, ambalo linaloletwa katika Baraza ambalo asitakiwe Makamu wa Pili wa Rais ajiuzulu. *(Makofi).*

Sasa unajua mimi ninataka niwaambie wenzangu Mhe. Naibu Spika, jambo ukilizungumza sana na likizoeleka, sasa hata yule ambaye unamwambia, anajua hili jambo ni jambo la kawaida. Hatujulikani wakati gani tupo *serious* katika kufanya kazi wala hatujulikani ni wakati gani tunaitaka Serikali ifanye kazi zake. Sisi tumekuwa tumo katika nyimbo za kawaida tu.

Kama ninavyozungumza Mhe. Naibu Spika, tumeanza kuzungumza kidogo hapa swahiba wangu mwana-Afro Shirazi hapa vizuri sana, yapo mambo hayajatekelezwa Makamu wa Rais ajiuzulu, ukija kwenye Mswada hili halikufanyika Makamu wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, ninasema sote tuna wajibu wa kuisimamia Serikali hii, na sote hatukuridhika na suala lililofanywa na wafanyakazi wa Ofisi ya Nyaraka. Hata mimi sikuridhika Mhe. Naibu Spika, kwa sababu vitendo kama hivi vikianza sehemu moja, basi nina imani kwamba sehemu nyengine pia vitaendelea. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, mimi juzi wakati ninachangia taarifa za kamati; nilichangia taarifa ya Kamati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi hapa na nikawaambia kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi walilamika juu ya eneo lao la Maruhubi kuchukuliwa na wananchi.

Mimi nikamuomba Mhe. Waziri kama eneo linachukuliwa na wananchi na wewe kama Waziri, mimi sikumtaka Jihad ajiuzulu kabisa, sikumwambia Jihad ajiuzulu kwamba ameshindwa kusimamia eneo la Maruhubi, ambalo ni eneo la Serikali kuchukuliwa na wananchi. Kwa sababu unatakiwa mtu umuelekeze lile jambo unalomuelekeza akalifanyie kazi.

Sasa hii tofauti na wenzetu, na ninafikiri kama wangelikuwa wanajua hili wao au ingekuwa ni Waziri wa Serikali wa upande mwengine ingekuwa ni sewe, lakini nilimuelekeza Mhe. Jihad nikamwambia kama kuna tatizo Maruhubi, basi hamuoni haja ya Wizara lile eneo kulirejesha Ardhi, lile eneo likagaiwa kwa shughuli nyengine ili hayo madume ya mbegu yakapelekwa katika maeneo mengine kuyafanyia kazi, lakini jawabu niliyojibiwa Mhe. Naibu Spika, ilikuwa ni jawabu la mkato.*(Makofi).*

Kwa kweli jawabu la kuonekana kwamba Serikali au wasimamizi wa Serikali wapo tayari kuisaidia Serikali hii. Hii ilivyoonekana Mhe. Naibu Spika, ninasema sana kwa upande mmoja tu. Alinijibu hao watu waliokuwapo hapo kiburi chao unakijua!

Wewe ndiye Waziri, wewe ndiye tuliyekupa Wizara usimamie. Tunazungumza malalamiko ya maeneo au ya mali ya Serikali ambazo zinachukuliwa na wananchi, unaniambia unajibu kwamba kiburi cha watu unakijua, nitakijuaje. Utakijua wewe tuliyekupa dhamana ya Serikali kusimamia suala hili. *(Makofi).*

Sasa Mhe. Naibu Spika, ninasema kwamba suala la wizi katika Serikali hii limekuwa kubwa sana. Kama Wajumbe tunapiga kelele nyingi sana. Jana tulikuwa tumemaliza masuala ya madeski hapa kwamba hili hatulipendi, na kama hatulipendi, basi tunaiomba Serikali tunapozungumza haya masuala yafanyiwe kazi ili Wajumbe na sisi tufike pahala tujiridhishe. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, suala la wizi lipo kwenye pesa za Serikali, lipo kwenye mashamba ya Serikali. Sasa hivi tunaingia kwenye Nyaraka.

Sasa Mhe. Naibu Spika, sitaki kuchukua muda wako mkubwa sana. Niiombe Serikali kwa dhati kabisa katika hili, waiangalie ripoti, wasikilize hoja za Wajumbe, na hatimaye tuiombe Serikali kuifanyia kazi kwa kila ambaye amehusika kwa namna moja au nyengine katika wizi na upotevu wa nyaraka za Serikali, awe mtoto wa mjomba, awe mtoto wa shangazi, tunaomba haki itendeke na sheria ifuate mkondo wake.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi)***.**

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Ali Salum Haji tunakushukuru. Sasa nafasi tunampa Mhe. Hassan Hamad Omar baadae Mhe. Salim Abdalla Hamad na muda ukiwepo Mhe. Saleh Nassor Juma.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Naibu Spika, na mimi ninakushukuru sana kunipatia nafasi kuweza kutoa mchango wangu wa mawazo katika hoja tuliyonayo.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla,* aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati Teule juu ya upotevu wa nyaraka. Ni jambo kuwa halikujificha. Nimeshuhudia mwenyekiti wetu jana karibuni masaa matatu kasorobo anawasilisha ile ripoti. Mimi nilimuonea huruma sana kwa kazi ngumu aliyoifanya na kipato haina! *(Makofi).*

Ninasema kwa kazi ngumu aliyoifanya na kipato haina, kwamba kila tunavyozungumza ndani ya Baraza la Wawakilishi, basi kama tunatwanga maji kwenye kinu, hayakai.

Mhe. Naibu Spika, ripoti nyingi za Kamati Teule zinazoletwa katika Baraza hili, lakini hatuoni hatua muafaka zinazochukuliwa. Tunazungumza kwa upeo kabisa, lakini siku baada ya siku hatuoni hatua zinazochukuliwa. Sasa hivyo ilikuwa hata hili Baraza letu ambacho ni chombo kikubwa hichi cha wananchi kinadharaulika. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, kama wazungumzaji wenzangu waliopita wamezungumza kuwa nyaraka ni muhimu sana kwa nchi na maendeleo ya wananchi. Historia na kumbukumbu kubwa katika kuhifadhi nyaraka. Hata sisi hapa tupo ndani ya chombo hichi basi kila mtu ana *note book* yake ya kuandika haya kwa kuhifadhi, ili kama hana *note book* basi hilo jambo anaweza akalisahau. *(Makofi).*

Sasa sisi leo nyaraka zinachukuliwa tu kama karatasi za kufunga maandazi. Hili si jambo jema. Tunaiomba Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa kuwa macho zaidi na zaidi, bila ya hivyo nchi itakwenda na maji kama walivyozungumza wenzangu. *(Makofi).*

Ninasema hivyo kwa sababu ya msingi, nyaraka ni kumbukumbu, na sisi tunajifunza kutokana na nyaraka ambazo ni kumbukumbu, historia tunajifundisha kutokana na mambo hayo.

Kila mtu anazaliwa baadae anasoma historia, siyo kwamba kila anayesoma ile kwa sababu ameona, lakini ameona katika vitabu katika kujifunza. Na sisi tutapata kumbukumbu katika nyaraka hizo lakini naona Serikali inakwenda mchomo kwa jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, wametajwa watu hapa, watu watatu wametajwa hapa, akina Mwanakombo Ali, Mwanahawa na Humoud. Unaweza ukatajwa na jambo hili kuwa hukuhusika lakini aliyekuwemo hataki na asiyekuwemo haiingii.

Kwa hivyo kwa sababu wao wametajwa wanaweza kuwa wao ni mashahidi katika kuipatia ushahidi Serikali. Naomba jambo hili lifuatiliwe na Serikali, baadae ichukue taratibu za kisheria na sheria ifuate mkondo wake.

Mhe.Naibu Spika, ukitaka kuangalia kama nyaraka zina umuhimu, aangalie tu watu wanaozozana au kugombana kwa ajili ya sehemu ya shamba au ardhi, baadae mtu yule akawa na nyaraka na akafuatilia jambo lile mpaka akapata haki yake. Unakwenda ushahidi wa nyaraka, na aliyekuwa hana nyaraka anakosa, mwenye nyaraka anapata haki yake. Kwa hivyo nyaraka zina umuhimu sana katika nchi na katika kumbukumbu za watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, ninaamini sana kama Serikali ina mkono mrefu. Hata mtu alizungumza hapa kama yupo Oman, yupo wapi, Serikali ikitaka dakika mbili tu itampata na atakuwa na mambo ya kujibu katika tuhuma anazotuhumiwa.

Lakini kama haitoshi Mhe. Naibu Spika, katika sehemu zetu za kuhifadhi nyaraka ni lazima ziwe nzuri na ziwe na nafasi ya kuhifadhi yale mambo kwa utulivu kabisa.

Lakini utakuta nyumba ya kuhifadhi nyaraka hapo Kilimani, wenzetu waliokwenda kuchunguza ile sehemu haipo vizuri, zinatupwatupwa tu, na kitu wenyewe ni karatasi. Hii karatasi inafika wakati inaoza na hasa ikiwa hukuiweka katika utaratibu mzuri. Kwa hivyo tunaiomba Serikali iwe makini juu ya jambo hili la kuhifadhi nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, nipate kusema tena kuwa kuhusu uhifadhi wa nyaraka ni jambo zuri sana. Halafu hili jambo liwe makini kufuatiliwa. Leo mtu anahongwa shilingi elfu ishirini anakwenda kutoa nyaraka za Serikali. Ni jambo dhaifu na lisilokuwa na utulivu.

Lakini kwa nini hakuna ulinzi katika sehemu zetu za kuhifadhi nyaraka. Kwa nini kusiwe na ulinzi wa kutosha katika sehemu zetu za kuhifadhia nyaraka na jambo hili tunaliona ni muhimu sana. Sehemu ndogo ndogo tu hapo kuna walinzi kushinda kiasi, lakini jambo la nyaraka hili inakuwa hatuna ulinzi wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, sisi tunaomba Wawakilishi tuliopo hapa jambo hili lichukuliwe hatua na kitu kimoja tu kinachozungumziwa ndani ya jambo hili, ni nyaraka tu. Kila anayesimama hapa ni nyaraka tu, hakuna jambo jengine.

Hivyo Wajumbe wote wanaochangia na kuhimiza Serikali kuchukua hatua za kisheria kwa jambo hili. Kamati imefanya kazi nzuri sana kwa muda wa wiki sita, imefanya kazi zake, na tokea jana imetupa ripoti hii na sisi Wajumbe tuliichangia na tumeliona kwamba kuna jambo la ubadhirifu, kwa hivyo hatua zichukuliwe za kisheria na aliyehusika akamatwe na kuchukuliwa hatua atakapopatikana na hatia atiwe hatiani.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu huo kuhusu upotevu huu wa nyaraka. Ni kwamba Serikali yetu tunaihimiza sana na ifanye fungu la huruma, kwa sababu kama nilivyozungumza, kama sisi Wawakilishi kuliona jambo halikuchukuliwa hatua na jambo hilo ni la ukweli, basi inakuwa hatuna maana yoyote mbele ya jengo la Baraza la Wawakilishi hili na Serikali nzima kwa ujumla. Lakini wakati litachukuliwa hatua jambo kama hili, basi kama Hakimu anavyohukumu Mahakamani, akasema anatoa adhabu hii ili iwe ni fundisho kwa mtu mwengine na aliyeko nyuma atafuata mkondo, atakuwa mwoga.

Lakini kama tunavyozungumza hapa baadae tunaachia, basi kila siku tutazungumza na hakuna chochote kitakachokuwa, na tutakuwa hatuna maana yoyote, maana tunasema tu lakini hakuna jambo linaloshughulikiwa. Hii si nzuri na haingii akilini kabisa. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, tunaiomba Serikali, jambo hili lipo, tangu linanong'onwa mpaka limekuwa dhahiri, na chombo hichi na wananchi wote wanaona tunavyozungumza. Kwa hivyo litiliwe maanani na lifanyiwe haki yake ya kisheria, na aliyekuwa hahusiki aachiwe na aliyekuwa anahusika atiwe hatiani na Serikali ifanye mambo yake.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka kuzungumza hayo machache, naomba niishie hapo na ninaunga mkono asilimia mia juu ya mia ripoti ya Kamati Teule hii ya upotevu wa Nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, ahsante ninakushukuru. (*Makofi*).

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Hassan. Sasa nafasi tunampa Mhe. Salim Abdalla Hamad baadae Mhe. Saleh Nassor Juma na muda ukiwepo Mhe. Mgeni Hassan Juma.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya wakati sitozungumza yote niliyokusudia ili Mhe. Saleh Nassor Juma na yeye apate alau kuzungumza machache.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe shukurani kwa Mwenyezi Mungu kutujuulisha kuwa Zanzibar kuna nyaraka nyeti, tena za siri zimeibiwa.

Nishukuru sana Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa wakati mfupi, ambao kutokana na maelezo ninayoyaona haikukamilika ipasavyo.
Mhe.Naibu Spika, nimuhurumie sana Mhe. Waziri aliyehusika na kwenda kuona kuwa mambo ni kama haya aliyoyakuta.

Pili, niweze kutoa nafasi kwa Mhe. Saleh Nassor Juma, mimi nitazungumzia ukurasa wa nne, wa tano na wa sita kwa ufupi wa kitabu hichi cha ripoti, ambacho unakusudia kueleza ripoti ilivyofika, kesi ilivyofuatiliwa na yaliyokutikana.

Mimi moja kwa moja nianze na matokeo ya ukaguzi ambao ulijulikana ni kama ifuatavyo. Kuna vielelezo vya ma-*files* saba au *subject* saba vilivyofanyiwa utafiti kama *samples*, tukisema *sample* maana yake ni mfano tu. Hii ni kuashiria kuwa kuna mengi na mengi sana ambayo hayakufuatiliwa.

Mhe. Naibu Spika, sasa tukiangalia nambari moja tumeandika hapa *Edwin Death Record Series and Correspondents.* Na hapa makasha matatu, yaani *boxes*. Nyaraka zote zimeibiwa. Nyaraka za makasha

matatu au boksi matatu ni mengi. Bahati mbaya hapa hazikuelezwa, hatuzijui ni zipi na wala hatuzijui umuhimu wake, tumo katika kiza, tuione hivyo hii hali.

Pili, *ZA Record Series Arabic Manuscripts*, zilikaguliwa na kubainika kwamba ZA2 vitabu 9 vimeibiwa havimo na ZA3 vitabu vitatu vimeibiwa, jumla ni vitabu 12 hatuvijui ni vipi na umuhimu wake ni upi, lakini mpaka kitu kikiibiwa kina umuhimu wake mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, tukienda namba *3* ya *echo consular record series AA4* makasha mawili yameibiwa, *AA5/6-8* mafaili 3 yameibiwa. *AA5/ A 17* mafaili mawili yameibiwa. Halafu kuna *AA5/82 2A* na 2D zimeibiwa katika kasha lake*, AA5/91* namba 11 na namba 13 yameibiwa *AA5/86* faili nambari 15 limeibiwa.

Ni mafaili mengi yameibiwa, lakini hatuyajui ni mafaili gani na umuhimu wake ni upi. Mimi kwa sababu ya unyeti wa mafaili nilifikiria kila sehemu inayofanywa utafiti katika hiyo *sampling* tungelijua faili hili linahusiana na hiki na hiki ili tukajua ni wizi gani uliokuwa umeshatolewa, lakini ndio haukuelezwa. Tumeendelea hivyo mpaka mwisho, kwa sababu ya wakati Mheshimiwa mimi naomba nitoe fikra zangu.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, kutokana na maelezo yaliyopo ukurasa wa 7 ambayo naomba nisome kwa ruhusa yako, yaani kuhusu huyu ndugu yetu Khadija Iddi Mohammed. Yeye alieleza kuwa mwezi Novemba aliwahi kupigiwa simu na nambari ipo hapo ya simu, ikimtaka wakutane Kiembe Samaki, lakini hakwenda na kumjulisha Naibu Mkurugenzi wake. Utafiti ukafanywa ikaonekana simu hiyo ni ya Humoud.

Mimi hapa kiutaalamu inanipa mashaka, vipi mtu anakupigia simu humjui, hukutaka kwenda ikabidi uende kwa Mkurugenzi wala hukwenda popote pengine, ina maana kuna kitu ndani ya serikali kilichokuwa kinajulikana kinaendelea. Huyu mama alipopigiwa simu akaogopa, kwa sababu kuna kitu kakijua ndio akaenda kwa Naibu Mkurugenzi. Kwa maana hiyo, kuzungumza vyote hivyo nakusudia kusema kitu kimoja.

Waheshimiwa Wajumbe hii Zanzibar ni nchi na mambo haya yanahusiana hata na ubalozi. Nchi haiwezi kuwa nchi mpaka iwe na nyaraka zake zinazoifanya kuwa nchi. Nchi haiwezi kuwa na historia mpaka iwe na nyaraka zake zinazoifanya kuwa na historia. Mtu hawezi kumiliki kitu mpaka awe na ithibati zake. Kuibiwa kwa nyaraka hizi za siri, mimi silichukulii kuwa ni jambo rahisi kama wenzangu wanavyouliza kuwa kuna kundi limefanya hivi lichukuliwe hatua.

Mimi nasema kwa sababu ya huyu Khadija kumjua Humoud kabla ya kuwa anahusika asingekwenda kwa Mkurugenzi. Mimi nasema moja kwa moja kwamba ni lazima kuna mkono mkubwa unaohusika na haya, tena kisiasa, kuna mkono mkubwa unahusika na haya, tunaibiwa mambo yetu na ninaamini ni kwa muda mrefu sana. Haya ni mambo saba tu tofauti, na tumeona haya lakini kuna mengi kweli kweli.

Ninaamini tokea hapo mwanzo yalipokuwa yakitokea serikali ilikuwa inaelewa, na ninaamini yakifanywa kwa makusudi ili huu uhalali hasa historia na umakini wa hii Zanzibar upotee.

Sasa basi kwa sababu kuliibiwa na waliokuwa wakiingia na mikoba wanajulikana. Hivyo walivyoiba, serikali ifanye *the other way round,* warejeshe mali ya watu, wala hakuna msamaha, kufungwa au vyenginevyo hakusaidii chochote. *This is a political issue,* ni lazima itiliwe maanani sana. Halafu, je, itakuwaje nchi hii yenye ulinzi uliokithiri mpaka maboksi yaweze kuondoka, makasha yachukuliwe iwe serikali haijui yalisafirishwa wapi hayo, kuna njia ya chini kwa chini yalipitishwa hayo, kama walivyokuwa wakisafirishwa watumwa au na kadhalika, lakini naamini hii ilikuwa ni *issue,* na *issue* hii kama hatujaichukulia *seriousness*, tukaitaka serikali iwajibike kikamilifu kwa kuona kuwa *reverse action* imefanywa kwa kupata hizi nyaraka zetu, *Wallahi* nchi hii mwisho wake itakuwa ndio imeuzwa moja kwa

moja, na huko wenzetu wanakokusudia kuipeleka itafika, halafu sisi ndio tutakaokwenda kuhukumiwa kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, namaliza kwa kumpisha Sheikh Saleh Nassor, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Mjumbe, sasa tunampa nafasi Mhe. Saleh Nassor Juma, nadhani muda utamtosha na waliobakia tena tukijaaliwa Jumatatu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa hii kuweza kutia nyalio katika hii taarifa, kutiatia nyalio pamoja na kuchechemua kama nilivyoiangalia hii ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka.

Kwanza napenda nichukue fursa hii kuwapongeza Wajumbe kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. Kazi ya Kamati Teule Mhe. Naibu Spika, haina mambo mengi ya kusema, kwa sababu wanatumia *supporting documents*, *supporting documents* zimo. Nyaraka zimeibiwa na wameweka *supporting documents*, kwa hivyo sasa kazi ni ya serikali kuchukua hatua, lakini wao wamejitahidi wenzetu.

Kwa hivyo, Mhe. Mahmoud Muhammed na kamati yake tunawapongezeni sana kwa hii ripoti yenu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nyaraka ni kitu muhimu sana kwa usalama, historia, pamoja na uchumi wa nchi. Aliwahi kueleza Mhe. Omar Ali katika michango yake, kwamba nyaraka ni uchumi, nyaraka ni usalama na nyaraka ni historia. Kwa mnasaba huo Mhe. Naibu Spika, kama kuna kitu ambacho kinahitaji kutunzwa, kama kuna kitu kinahitaji kulindwa, kama kuna kitu kinahitaji kuenziwa basi ni nyaraka.

Inasikitisha sana Mhe. Naibu Spika, kwamba sisi walipa kodi wa nchi hii, tunatumia fedha zetu nyingi sana kuwaajiri watu katika idara hii, lakini hawatupi kile tunachokihitaji, kwa maana ya kwamba hawatufanyii kazi ya kutulindia nyaraka zetu.

Leo nyaraka zinaibiwa nyingi tu, kama alivyoainisha Mhe. Salum hapa. Kwa mnasaba huo walipa kodi wa nchi hii hatuko radhi kutokana na uzembe uliofanywa na watumishi.

Mhe. Naibu Spika, sisi hatuiambii serikali ifanye nini, kama kawaida yake, kwa sababu huwa tunaletewa Kamati Teule tunajadili, tunasema lakini matokeo yake serikali inakaa kimya kama haikuambiwa neno, lakini sisi kazi yetu ni kusema, huu ni uzembe mkubwa na hatua za kisheria zinatakiwa kuchukuliwa katika uzembe huu uliofanyika.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia umuhimu wa kutunza mambo haya na serikali lazima iwe makini katika kutunza hizo nyaraka zenye historia. Hivi karibuni mimi nilimpata *researcher* mmoja kutoka *America*, alikuja hapa anafanya PhD, akaenda katika maeneo ya nyaraka kutafuta historia ya Field Marshall John Okello na Mapinduzi ya Zanzibar. Yeye alikuwa akifanya *African History*.

Sasa moja alilokuwa akilitaka ni historia ya John Okello. Kaja huku kahangaika kakosa. Akaambiwa huyu John Okello alikuwa akikaa Vitongoji, akanifuata mimi ndiyo nikampeleka katika maeneo ya Vitongoji kwa bwana mmoja anaitwa Mzee Abdalla bin Juma wa Vitongoji Umangani pale, halafu nikampeleka kwa Mzee Maisara Mkoani Hospitali pale, kuingia tu kwa Mzee Maisara akapata historia ya kutosha kuhusu Field Marshall John Okello na Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba watu wanaohifadhi kumbukumbu hawana mambo haya, wanashindwa na Mzee Maisara, wanashindwa na Mzee Abdalla bin Juma pale Umangani.

Inasikitisha sana Mhe. Naibu Spika, kwamba Mzee Said Udende ambaye ni Marehemu anayajua Mapinduzi na anaijua historia ya Zanzibar kuliko *archives,* akienda hawayapati mambo kama haya, ikiwa hatukuwa makini Mhe. Naibu Spika, katika kuzienzi hizi nyaraka tulizonazo, napata wasiwasi. *(Makofi)*

Hivi karibuni upanga wa polisi uliibiwa wa dhahabu, tukahangaika wee na kutumia *Interpol* sijui kama ule tuliopewa ndio au sio, ndio serikali inalijua hili, sisi waasisi hatujui, sijui vyombo vya ulinzi wa usalama kama ule uliopatikana ndio au sio. Lakini jambo la historia kama upanga wa dhahabu unachukuliwa ni historia ya nchi inadhalilishwa kama vile, inaumiza sana Mhe. Naibu Spika.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ikiwa hatukuwa makini na wazembe kama hawa ambao wanapenyeza siri za nyaraka za nchi, keshokutwa watapeleka siri za usalama wa nchi, tukija tukitahamaki Rais wetu keshaibiwa.

Tunampenda sana Rais wetu, kama leo wamepenyeza siri za nyaraka katika *safe* hili la kuhifadhi nyaraka, kesho hawa watapenyeza siri za usalama wa nchi, matokeo yake Rais wetu ataibiwa. Tukikaa kidogo Makamu wetu wa Pili ataibiwa, hatujakaa vizuri Makamu wa Kwanza, tukija kuangalia hakuna yeyote aliyebakia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, katika hili mimi nadhani tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno. Haya sio maneno yangu, tendo siku zote hukidhi haja maridhawa kuliko neno Mhe. Naibu Spika.

Haja ikishughulikiwa kwa matendo hupatikana wepesi, lakini ikishughulikiwa kwa maneno huchelewa kama sadaka. Shaaban Robert 1947, nilikuwa nanukuu hapo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama siku zote tutaletewa taarifa za Kamati Teule tukiisema serikali hapa ichukue hatua ikiziweka kwenye makabati, matokeo yake hatutokuwa na nchi tena katika nchi hii. Itakuwa Fungu Mbaraka linachukuliwa Tanganyika, Pemba itachukuliwa Kenya, sijui tukija tukitahamaki sisi ni sehemu tu pengine ya Buguruni hapa, hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani katika hili ni lazima tuwe makini, na kwa sababu mimi sasa hivi natokea safari, nilikwenda Pemba kidogo kutokana na kufiliwa, mambo ya kusema siwezi sana.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, kwanza kwa michango mizuri, lakini pia kwa kunipa ushirikiano wenu tangu asubuhi hadi sasa hivi.

Sasa naomba nitoe taarifa moja muhimu, kwamba wenzetu waliotuandalia semina wameshakuwa tayari na wanataka tukishamaliza kusali chakula kiko hoteli hapo cha kujihudumia mwenyewe, unachotaka utachukua ule.

Tukimaliza saa 8:00 kamili wanataka waanze ili saa 11:00 kamili tumalize. Wameshachukua tiketi ya ndege hiyo ili waondoke. Kwa hivyo, naomba sana tukishamaliza kusali, tule tupande juu tukafanye semina, saa 10:00 tumalize ili saa 11:00 tuwaruhusu waende zao.

Baada ya maelezo hayo, tumebakiwa na wachangiaji watatu ambao nategemea roho zikifika Jumatatu, ataanza Mhe. Nassor Salim Ali, Mhe. Mgeni Hassan Juma na atamalizia na Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

Baadaye watafuatia mawaziri watatu ambao watajibu hoja. Kwanza ni Mhe. Haroun Ali Suleiman; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, pili Mhe. Haji Omar Kheri; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, na wa tatu ni Mhe. Mohammed Aboud Mohammed;

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na baadaye kama Mhe. Mwanasheria Mkuu na yeye ataongezea, baadaye tutamwita Mhe. Mwenyekiti atafanya majumuisho.

Baada ya maelezo hayo sasa naahirisha kikao chetu hadi siku ya Jumatatu tarehe 30 Machi, 2015 saa 3:00 za asubuhi.

*Saa 6:51 mchana Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 30/03/2015 saa 3:00 za asubuhi)*